# Akaanza Kutoka Musa



Mwongozo wa awali wa kukusaidia kusoma na kuelewa maandiko matakatifu

**TOLEO LA KWANZA**

Shemeji Melayeki

**Akaanza kutoka Musa ©2021 Shemeji Melayeki**

**Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi isipokuwa kwa nukuu mbalimbali na matumizi ya kufundishia.**

SIMU: +255 714 548 565

+255 763 965 297

Email: *shemeji.melayeki@gmail.com*
YouTube: *Shemeji Melayeki*
Instagram: *apostle_shemeji_melayeki*
Twitter: @*melayeki*
Facebook: *Ap Shemeji Melayeki*

**ISBN - 978-9976-5427-8-3**

Kimepigwa chapa na: **CLIMAX SOLUTIONS – ARUSHA**

**+255 658 288 054**

**+255 687 699 862**

# YALIYOMO

TABARUKU ........................................................ iv
SHUKRANI........................................................ v
UTANGULIZI ........................................................ vi
SURA YA1 ........................................................ 1
*MISTARI PENDWA* ........................................................ 1
SURA YA 2 ........................................................ 4
*UNATAFUTA NINI KWENYE BIBLIA?* ........................................ 4
SURA YA3 ........................................................ 9
*KILA MTU ANA MAFUNUO YAKE*........................................ 9
SURA YA 4 ........................................................ 14
*MAANDIKO MATAKATIFU NI NINI?*........................................ 14
SURA YA5 ........................................................ 21
*KUNYONGA MISTARI NA MUKTADHA* ........................................ 21
SURA YA6 ........................................................ 26
*LENGO KUU LA MAANDIKO MATAKATIFU* ........................................ 26
SURA YA7 ........................................................ 32
*UNASOMA KAMA YESU AU FARISAYO?* ........................................ 32
SURA YA8 ........................................................ 39
*ILI LITIMIE NENO LILILONENWA* ........................................ 39
SURA YA9 ........................................................ 49

*KUYAHUBIRI KAMA YALIVYOTIMIA: PETRO* ................. 49

SURA YA10 ........................................................................ 57

*KUYAHUBIRI KAMA YALIVYOTIMIA: PAULO* ................. 57

SURA YA11 ........................................................................ 70

*UBAKI UKIMWONA MWANA PEKEE* ................................ 70

SURA YA12 ........................................................................ 79

*KUNANI MATHAYO HADI UFUNUO?* .............................. 79

SURA YA13 ........................................................................ 90

*AKAANZA KUTOKA MUSA* ................................................ 90

SURA YA14 ........................................................................ 98

*MATHAYO, MARKO, LUKA NA YOHANA* .......................... 98

SURA YA15 ...................................................................... 105

*MATHAYO NA AGANO LA KALE* ................................... 105

SURA YA16 ...................................................................... 117

*MATENDO YA MITUME NA AGANO LA KALE* ............... 117

SURA YA17 ...................................................................... 140

*NYARAKA NA AGANO LA KALE* .................................... 140

# TABARUKU

Kwa jamii ya waaminio wenye kiu ya kumjua Mungu katika uhalisia wake, hasa wale waliokuwa wameshikilia ufahamu wa Mungu usio sawa.

Kwa watu wote wenye kiu ya kumjua Mungu na kizazi chenye maswali yanayohitaji uchambuzi wa maandiko utakaosaidia kuimarisha mahusiano yao na Mungu.

# SHUKRANI

Kwa Mungu ambaye ni Baba wa roho zetu na mwasisi wa maisha tuliyonayo, nakushukuru kwa utulivu wakati wa kukiandaa kitabu hiki.

Kwa familia yangu, mara nyingi nimekuwa macho usiku wakati wamelala, kwa utulivu mkubwa walionipa. Mke wangu Neema amekuwa msaada mkubwa katika kuhakikisha nafanikisha uandaaji wa kitabu hiki.

Kwa timu ya watu waliojitolea kujifunza kupitia kwangu kwenye huduma ya Global Family Gatherings, madarasa ya God’s Standards na wengine wengi kwa njia ya mitandao ya kijamii, wamekuwa sababu ya kunifanya nijitume zaidi.

Kwa wadau wanaofanya huduma pamoja na mimi kwa njia ya sadaka zao ili kuhakikisha kazi hii haikwami, wamekuwa waaminifu kwa rasilimali zao ili kweli hii ienee zaidi.

# UTANGULIZI

Tumefika hapa tulipo kwa sababu ya Matumizi mabaya ya maandiko. Ukisikia mwalimu wa uongo, nabii wa uongo, mtume wa uongo, na mambo yanayofanana na hayo ni matokeo ya matumizi mabaya ya maandiko. Hawa si watu wanaosoma magazeti kanisani au wanaoutimia Gita ya Wahindu au Quran ya Waislamu au Tripitakas ya Wabuddha bali ni watu wanaotumia Biblia. Yes, wanatumia Biblia. Mkristo hawezi kudanganywa kwa kutumia gazeti la udaku maana ataona wazi wazi akidanganywa lakini pia mhubiri anaweza kuigeuza Biblia kama kitabu cha udaku kama asivyotumia inavyotakiwa.

Ni vizuri tukawa waangalifu kwa baadhi ya mambo tunayoyasema na kuwaambia watu wengine kwa habari ya Maandiko. Katika mfululizo huu nitakujulisha mambo kadhaa yatakayokusaidia kuyapa HESHIMA Maandiko badala ya kuyatumia vibaya.

Chimbuko lolote la udhaifu wa tafsiri ya maandiko ni matokeo ya kutotaka kujifunza kwa uhalisia na UMAKINI habari za maandiko matakatifu. Kwa muda

mchache ambao nimehubiri kwa kutumia Biblia nimegundua ya kwamba habari nyingi tulizonazo hatujui hata zimeandikwa wapi. Nyingi ni zile ambazo tulimsikia mhubiri akisema, na sisi tukapenda na sisi tukawaambia wengine nao wakawaambia wengine.

Ukweli ni kwamba ukianza kwenda kufanya 'study' mwenyewe; Kuna vitu hutakuja kusema tena, kuna uropokaji utakufa kabisa. Mtu akishasema utatamani na wewe kujionea kama MAMBO HAYO NDIVYO YALIVYO (kama watu wa Beroya), mdomo wako utauwekea lijamu utakapotaka kusema jambo kutoka kwenye maandiko. Kwa sababu ya watu wengi kutaka kujibu "HARAKA" wamejikuta wamepotosha wengi. Si vibaya haraka hasa kama umeshakiki kwamba huo ni ukweli bila kutumia habari za kusikiasikia tu.

Lakini siyo tu kujibu haraka pia kutaka kuonekana kuwa UNAJUA na kulinda heshima ya ujuzi kama MTUME, NABII, MWINJILISTI, MWALIMU NA MCHUNGAJI au pengine tu "MTUMISHI". Kwa experience yangu, kadri ninavyojifunza juu ya maandiko matakatifu hali ya kutaka kujibu haraka imeniishia kabisa hasa kama swali nililoulizwa sijawahi kuulizwa. HII NI KWA SABABU MAANDIKO MATAKATIFU YANATAKIWA KUPEWA HESHIMA YAKE.

Katika mfululizo huu nitakuonyesha baadhi ya mambo yaliyonisaidia, yanayoendelea kunisaidia huku najifunza kusaidika zaidi.

# SURA YA 1

## *MISTARI PENDWA*

Kuna mistari ya Biblia naiita "MISTARI PENDWA" Hii mistari ni maarufu sana. Yaani ukitaja kitabu cha kwanza mtu anachokumbuka ni huo mstari.

Sasa hii mistari pendwa ni mstari “ILIYONYONGWA”

Kusema iliyonyongwa namaanisha nini? Hii mistari imekuwa kama ramani ya kutafsiri Biblia. YANAJITAFSIRI YENYEWE UNALAZIMISHA

KUPATA MAANA MULE MULE. UNAJIFUKIZA MSTARI.

Ukitaja Leo kitabu cha Ayubu watu wengi akili zao zitakimbilia ***Ayubu 22:21 "Mjue sana Mungu ili uwe na amani..."***

Ghafla utarukia mbele bila kuangalia nani kasema, kwa nani, kwa sababu gani? Si ajabu utaanza kusema "AYUBU KASEMA..." Cha ajabu maana ya kumjua Mungu italazimishwa itoke kwenye huo mstari tena mwingine atakuambia "AYUBU ALIMJUA MUNGU" bila kujua kuwa AYUBU ALIKUJA KUSEMA HAKUMJUA MUNGU (Ayubu 42)

Kwa sababu hatuna Tabia ya kusoma MISTARI JUU YAKE, MAANA NDANI YA MSTARI NA HATA BAADA YA MSTARI ili kujua mazingira yote ya Neno kabla hujaanza kupanua MAELEZO yaliyoko kichwani mwako.

Kwa mara ya kwanza nasoma kitabu chote cha Ayubu nilishangaa kuona kuwa Maneno hayo hakusema Ayubu bali Elifazi na alikuwa anamzodoa kuwa hamjui Mungu mbali na hayo huko juu alikuwa akimchana kuwa Yeye ni mtu mwovu, pengine amewaonea wajane, yatima na na kadhalika ndiyo maana kapatwa na hayo. Hivyo anashauri amrudie Mungu.

Baada ya kusoma kitabu chote nikaona tu siyo kwamba walimkosoa tu Ayubu (wale rafiki zake watatu) lakini pia wao walikosolewa kuwa wamekosea na kijana mdogo anayeitwa Elihu na Mungu pia.

Elihu alimkosoa Ayubu, Elifazi, Sofari na Bildadi. Mungu naye pia aliwakosoa wote.

Hapo nikaanza kufikiri kuwa SITAKIWI KUCHOTA TU CHOCHOTE KWENYE KITABU HICHO BILA KUJUA "WALICHOREKEBISHWA NI NINI NA KIPI KILIKUWA SAHIHI"

Lakini ukitembea na Mistari Pendwa Utarukaruka na kupata mapooza, Utapiga Ayubu 1:1-2, utakimbilia 22:21, utaanza 33:14-15, utakimbilia 42:1-2, HALAFU UTAHISI UMEELEWA.

Nitakayo kumaliza nayo ni hivi. Ukisoma kitabu chochote kwenye Biblia usitafsri mstari kama kisiwa. Mistari na SURA zina uhusiano, Sura kwa SURA uhusiano, kitabu kwa kitabu zina uhusiano, Agano kwa Agano zina uhusiano.

HIVYO, USINYONGE MSTARI MMOJA, ELEWA SURA YOTE, ELEWA KITABU CHOTE...

Una haraka ya kwenda wapi ndugu yangu?

# SURA YA 2

## *UNATAFUTA NINI KWENYE BIBLIA?*

Hivi unavyochukua Biblia na kutaka kusoma huwa unatafuta nini? Hilo ni swali muhimu sana

Mwaka 1999 ndiyo mara ya kwanza kuamua kwenda kanisani na kufuata utaratibu wote ulionifanya

niwe sehemu ya kusanyiko. Lakini baadaye niligundua kuwa bado nilikuwa tu mtu wa kawaida na hakukuwa na tofauti.

Mwaka 2001 na 2003 nikawa na matukio mengi sana ya kuongozwa sala ya toba. yaani ilitegemea kama kaja mhubiri mpya na katika kutaja dhambi ghafla akataja yangu mojawapo au amehubiri habari za siku za mwisho na nikajikuta nina hofu hivyo akiita watu mbele naenda hata kama nilikuwa mwenyewe

Kwa hiyo "Ee Bwana Yesu, Mimi mwenye dhambi ninakuja mbele zako.... " Nimezisema NYINGI SANA...

Miaka ya 2004 nikaamua kuanza kuwa serious na Injili na maombi nikiwa na rafiki yangu mmoja. Ninachokikumbuka ni style yetu ya kuhubiri. yaani kwanza TULIKUWA tunatafuta kujua shida za watu wa mahali fulani...kabla hatujaenda na utadhani waalikaji walikuwa wanajua lengo letu... yaani utaambiwa shida ya Fellowship au Shule au kanisa tuliloenda hadi basi, lakini utaambiwa kama wanasikitika hivi wala sio wanasengenya. Halafu watamalizia "Mtumishi Mungu akutumie tu kwa kweli" Ikiwa ni semina ya siku 2 na kuendelea utapata cha kuhubiri zaidi maana wakati wa chakula wale wahudumu watakupa points za kukazia kesho *indirectly.*

Yaani wakati wa chai au chakula utapewa heko na umbea pia...

"Yaani mtumishi Leo umegonga haswa, Roho alikuongozwa kweli, utatajiwa mambo chungu nzima kuanzia shida ya viongozi, mpaka waumini. Hapo kesho ibada itanoga. Maana utapita mule mule. Ukisikia "Sema Tupone" unajua sasa Injili imekolea. Kumbe kuna watu umepewa mawe uwaapige. ikawa style bhana. Ukitaka kwenda sehemu unapata details kwanza, ukisimama mbele unawatwanga watu mpaka wengine wanaangua kilio wakati wa mahubiri. Na watu watasema, "This man is on fire" Hapo umepanda na mistari uliyopangilia. Yaani kuna wakati ukisema tuombe shule au kanisa zima ni kilio. Kilichonisumbua ni kwamba watu hao baada ya muda wako vile vile na pengine wamekuwa WABAYA zaidi. Shida ni nini?

Nilikuwa nikienda kwenye mikutano ya akina Bonnke, na wazungu wengine waliokuwa wanakuja Arusha nilikuwa nashangaa sana. Nilidhani hata wazungu hawana Injili ya kweli kwa sababu waling'ang'ania kuzungumza habari za Yesu kama vile hawajui kama kuna uchawi Afrika, laana za ukoo, utoaji mimba, uzinzi na vitu kama hivyo. Nilikuwa najisemea, "These guys can't hit problems" Kwa nini hawagusi matatizo ya watu? Kilichonishangaza hata WACHAWI walikuwa wanaokoka kwenye mikutano yao.

Nilitaka amsha-amsha, yaani....

Baadaye nikamsoma kidogo Paulo na Petro walivyokuwa wanahubiri, nikashangaa sana. Paulo anaenda mji imejaa sanamu, anakomaa kufundisha KUTESWA KWA YESU, KUFA NA KUFUFUKA KWA AJILI YA ONDOLEO LA DHAMBI. Watu wamrejee Mungu kupitia Yesu Kristo. Kichwa kikaanza kuniuma, ya nini hii Paulo? Yaani unajua mimi ningeanza Mistari iliyojaa kichwani juu ya "Ole za kuabudu sanamu, na ubaya wa madhabahu zao" yaani pasingetosha.

Lakini akina Paulo walituliza munkari, wakafunua maandiko Taratibu bila haraka na watu wengi waliokoka. Nikapunguza kusoma vitabu vya Agano la Kale ili nione kile walichokuwa wanaona. Baadaye ikanisaidia sana. Baada ya muda nikaanza kujikita kwenye kufundisha habari za Kristo Yesu japo kwa kiwango cha ujinga fulani lakini angalau nilikuwa naonyesha jambo kuhusu Yesu na WOKOVU wake kwa njia ya Mauti yake na matokeo ya kazi hiyo. Msaada mkubwa uko hapa. USIPOELEWA MAANDIKO YA AGANO JIPYA, MAANDIKO YA AGANO LA KALE YATAKUSUMBUA ZAIDI, MAANA AGANO LA KALE MAMBO MENGI YAKO KAMA MIFANO, VIVULI, MAELEZO JUU YA MAMBO YAJAYO hasa yanayohusu Kristo na WOKOVU wake kwa watu wote.

Ukishajua hayo, Agano la Kale linaanza kuwa wazi Taratibu na hata Kristo Yesu utamwona akizungumziwa sana. Lakini usipoelewa yaani Kila UTAKACHOKIONA KULE YANAKUHUSU kwa namna isivyo sawa sawa. Kama ni Mhubiri utakuwa unakusanya Mistari ya kuwagongea watu ukidhani watabadilika kumbe hakuna kitu.

Yesu alisema katika ***Yohana 5:39***

***[39] Mwayachunguza maandiko [Ya AGANO LA KALE], kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia.***

Kama Yesu bado hajawa wazi kwako, Utajitesa na zaidi sana utawatesa wengine na kazi yako itakuwa ya kujilisha Upepo. Ushauri wangu ni kwamba kama una mpango wa kusoma Biblia kwa lengo la kujifunza ANZIA AGANO JIPYA. Na huko ndani utaona Agano la Kale lilivyozungumziwa. Just be DILIGENT AND RELAXED, HUKU UKIWA TAYARI KU UNLEARN MATANGO PORI.

# SURA YA 3

## *KILA MTU ANA MAFUNUO YAKE*

ജ൫

Katika sehemu hii nataka nizungumze kidogo juu ya kichaka kinachoitwa MAFUNUO. Hapa wengi wamelaza ujinga na kupeleka likizo ufahamu. Huyu ana ndugu yake mmoja anaitwa "HILO

FUNDISHO SI LANGU" au sijaitiwa hayo. Hayo ni baada tu ya kugundua kuwa tafsiri sahihi ya maandiko umepukutisha udanganyifu ulioshikilia ghafla watu wanakimbilia hivi vichaka viwili.

Siyo kwamba mimi niliruka "Big No" pengine mimi nilikuwa napotea kabisa. Tena nilikuwa napotelea pabaya. Mimi nilikuwa na "specialize" kabisa. Kuna wakati nilikuwa najiita "Apostle of Money" yaani nikisoma Biblia naona Hela Tu. Yaani hata kumfufua Lazaro natafuta kama kuna mchongo karibu na kaburi. Aisee I was lost. Yaani nilifika mahali naweza kusema maneno "KAMA HAUNA HELA INAWEZEKANA HAUNA MUNGU" So, ridiculous. Kuna wakati nikajiita Mwalimu wa kusudi, hapa nilinyonga mistari kweli kweli. Natafuta tu kusudi tu. kuna wakati "Vision au Maono" yaani naweza kufundisha semina nzima hata Yesu Kristo sijamtaja hata kidogo. Nikimtaja uwe na uhakika kazi yake ya ukombozi hutaisikia nikiitaja. Niliwahi hata kusema "USIPOJUA KUSUDI LAKO DUNIANI, MUNGU ATAKUHUKUMU"

Just foolishly because I didn't know.

Kutapika hayo matango pori inahitaji Moyo wa Utayari na kutaka kujua ukweli halisi hasa kwa lengo la kujifunza. Sasa, shida ya mafunuo ni yale maneno tunayoyahisi ni ya kweli kutokana na tulichokisoma hata

kama hakuna sehemu imeandikwa. Hayo mambo ndiyo "punchlines".

Nitakupa mfano: Unasoma mstari umeandikwa

***Luka 24:46 [46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;***

Ghafla unaanza ***"Inawezekana biashara yako imekufa Leo itafufuka, leo ni siku ya tatu yako"***

Lakini Mwandishi alikuwa na NIA NYINGINE KABISA alivyoandika Maneno hayo. lakini wewe unaona kama anachelewa and you want to talk about Business.

Ghafla lengo la kufufuka kwa Yesu kwa Muktadha wa MWANDISHI unapotezwa na mwili wa Kristo unakuwa umenyang'anywa lengo la maandiko hayo.

Mfano 2: "***Matendo ya Mitume 13:36 [36] Kwa maana Daudi, akiisha kulitumikia shauri la Mungu katika kizazi chake, alilala, akawekwa pamoja na baba zake, akaona uharibifu."***

Ghafla tunahama key, ***"Hautakufa kabla tunatimiza kusudi la Bwana"***

Hapo nimesema kwa ufupi sana. lakini ni vizuri sana. kabla hujalazimisha mstari uendane na fikra zako ni vyema ukajua, MWANDISHI ALIKUWA

ANAMAANISHA NINI, KWA WATU GANI, KWA SABABU GANI, ILI UPATE NIA YAKE.

NB: NIA YA MWANDISHI NI YA MUHIMU KULIKO NIA YAKO. SI WEWE ULIANDIKA HAYO MANENO, DO NOT EDIT, UNDERSTAND HIM.

Hapo sijazungumzia Mistari maarufu iliyochomolewa "Pasipo maono watu huacha kujizuia" hapa wengi wengi hawataki hata kusoma (b) yake. (Mithali 29:18)

Na ndugu yake, "Ajianavyo mtu nafsi yake ndivyo alivyo ile story imekaa kushoto sana" Mithali 23:7 nani anajiona, kwa nini?

Na baba lao "Iandike njozi katika vibao" njozi gani? Kwa nini? Who cares, unahama tu unaanza kusema ANDIKA MAONO yako. (Habakuki 2:2-4) hapo mbele mwenye haki kuishi kwa imani ni kazi nyingine.

Hapo bado hujapitia "Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu" Fil 4:13 Bila kujiuliza hayo "mambo yote" ni mambo gani?

Kwa kanuni chache nilizokufundisha juu ya kuyaheshimu maandiko utagundua vingi ukianza kufuatilia hiyo Mistari. Ni vyema kuepuka KUFANYA SPECIALIZATION AND DIVISION OF LABOUR. (Yaani kuchagua kuuelewa Biblia kwa mrengo fulani).

Haya mambo ya kujiita, Mwalimu wa Maombi, Nabii wa uchumi, Mwalimu wa Roho Mtakatifu, Nina wito wa wanawake, Mara Mwalimu wa single ladies HUWEZI KUIJUA KWELI YOTE. **UTAKUWA BIASED.**

Paulo, Petro, Filipo, na Yesu Kristo mwenyewe nenda kaangalie walivyoipa heshima maandiko.

***They had the same CORE MESSAGE ALL OVER..***. Na ujumbe wao ndiyo wetu...hatuwezi kujenga msingi mwingine.

# SURA YA 4

## *MAANDIKO MATAKATIFU NI NINI?*

Biblia unayoiona leo, siyo Biblia iliyokuwepo zamani.

Mitume wa Yesu Kristo hawakusoma.

1. Mathayo hadi Ufunuo wa Yohana,

2. Hawakusoma Vitabu vyenye Sura na Mistari kama sisi.

Kitabu ambacho Yesu na Mitume walitumia (hata Mafarisayo na Masadukayo) ni vitabu ambavyo tunaviita vya Agano la Kale yaani Mwanzo mpaka Malaki.

Hivi waliviita Maandiko Matakatifu.

Ukikuta sehemu yoyote kwenye Mathayo hadi Ufunuo "Maandiko Matakatifu" yametajwa ujue ni Mwanzo hadi Malaki.

Angalia.

***2 Timotheo 3:15***

***[15]na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu.***

Wakati Paulo anaandika Waraka huu hata Mathayo haikuwepo.

Angalia ***Warumi 1:1-3***

***[1] Paulo, mtumwa wa Kristo Yesu, aliyeitwa kuwa mtume, na kutengwa aihubiri Injili ya Mungu; [2] ambayo Mungu amekwisha kuiahidi kwa kinywa cha manabii wake katika maandiko matakatifu; [3] yaani, habari za Mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili,***

Hii ina maana habari za Yesu zilihubiriwa na Paulo kwa kutumia MAANDIKO hayo na kufundisha habari za Yesu Kristo kama **ahadi**.

Angalia Yesu alichosema ***Yohana 7:38-39***

***[38] Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. [39] Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa.***

Hii ina maana Habari za Imani na Roho Mtakatifu ni zilizungumzwa kwenye Mwanzo hadi Malaki.

Huwa unaona hivyo?

Jambo lingine ni kwamba vitabu hivyo havikuwa vimekusanywa sehemu moja kama leo tunavyotumia sisi pale yalikuwa yanahifadhiwa mbalimbali, mathalani Zaburi peke yake, Isaya peke yake n.k. vikiitwa "chuo" au "scroll" kwa Kingereza.

Angalia ***Luka 4:16-17***

***[16] Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome.***

***[17] Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palipoandikwa.***

Alitafuta maana hakikuwa na mistari wala sura kama leo sisi tunavyosoma.

Karne ya 13 Stephen Langton ambaye baadaye alifanya askofu wa Canterbury ndiye aliyegawa Biblia katika Sura tunazoziona leo. Miaka 300 baadaye yaani karne ya 16 Robert Estienne aliweka "milango au Mistari. Lengo lao ilikuwa ni kurahisisha kunukuu maandiko kwani mwanzo hayakuwa kwenye sura na mistari. Kitabu pekee kilichokuwa na mgawanyo ni Zaburi. Ndiyo maana kwenye matendo ya mitume Luka alinukuu Zaburi ya Pili.

***Matendo ya Mitume 13:33***

***[33] ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu ahadi hiyo, kwa kumfufua Yesu; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili, Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa.***

Hii inapatikana ***Zaburi 2:7 [7] Nitaihubiri amri; BWANA aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa.***

Kwa sababu ya kutokuwa na mistari na sura walikuwa wanataja sura kwa matukio yaliyofanyika. Angalia jinsi Yesu alivyotaja kitabu cha Kutoka...

***Luka 20:37***

***[37] Lakini, ya kuwa wafu hufufuliwa, hata na Musa alionyesha katika sura ya Kijiti, hapo alipomtaja Bwana kuwa ni Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo.***

Angalia sehemu ya sura ya Kijiti. (a passage about the burning bush)

***Kutoka 3:2,15***

***[2] Malaika wa BWANA akamtokea, katika mwali wa moto uliotoka katikati ya kijiti; akatazama, na kumbe! Kile kijiti kiliwaka moto, nacho kijiti hakikuteketea.***

***[15] Tena Mungu akamwambia Musa, Waambie wana wa Israeli maneno haya, BWANA, Mungu wa baba zenu, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amenituma kwenu; hili ndilo jina langu hata milele, nalo ni kumbukumbu langu hata vizazi vyote.***

Wakati mwingine iliwabidi wataje tu "kama nabii Isaya alivyosema" au nabii fulani alivyotabiri, au Musa alivyoandika n.k. kisha Maneno hunukuliwa. Yesu alipoingia hekaluni hakuwa Biblia kama za kwetu ilimbidi atafute sehemu anayotaka kusoma kwenye Chuo cha Nabii Isaya. (au kitabu cha Isaya kikiwa peke yake)

***Luka 4:17***

***[17] Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palipoandikwa,***

Siyo kama Leo tunawahi tu kusema "Hiyo ni Isaya 61"

Malengo ya Stephen Langton na Robert Estienne hayakuwa mabaya lakini matumizi ya kazi zao zimekuwa mbaya.

Watu wengi hawasomi tena Biblia kwa mtiririko wake na kuelewa MWANDISHI alikuwa anamaanisha nini. Ni mwendo wa KUNYOFOA kamstari fulani na kutafuta maana iliyoko kichwani kwako hata kama MWANDISHI hakumaanisha hivyo. Kama ambavyo huwezi kutafsiri barua ya mpenzi wako kwa KAMSTARI KAMOJA bali utasoma barua yote ili uelewe kusudi/dhumuni la uandishi wake? Kwa nini kwenye Biblia tunatembea na Mistari Mistari ambayo hatujawahi kuyafanyia study? Hebu fikiria mpenzi wako kaandika barua na ukakumbia kuchukua kamstari KAMOJA katikati kanakosema "BASI MIMI NA WEWE BASI TUACHANE" unaanza kuwapigia ndugu zake, rafiki zako kwa kutaka kukuacha wakati umeshamtambulisha hadi nyumbani. Siyo ungesoma barua nzima? Imagine barua ingekuwa inasema "KABLA SIJAJA KWAKO, KULIKUWA NA NDUGU TUNATAKA KUFUNGA NDOA. LAKINI KUNA

BAADHI YA MAMBO TULISHINDWA KUAFIKIANA. NIKAONA ISIWE SHIDA NIKAMWAMBIA **BASI MIMI NA WEWE BASI TUACHANE**. LAKINI NIMEKUPATA WEWE, NINA AMANI KABISA, TUTAISHI VIZURI"

Ungetulia na kusoma yote usingechanganyikiwa wala KUSABABISHA madhara yoyote. Unaposoma tu kitabu cha hadithi, huwa unaanza katikati? Siyo lazima uelewa habari za nyuma kwanza? Kama unataka kuelewa Waraka wa Paulo kwa Wakorintho, kama hujaanza kunukuu mistari angalau uwe umeshasoma Waraka wote kwanza. Alikuwa na lengo gani? Wakorintho walikuwa na shida gani? Alitatuaje? Alitumia Maneno gani? Na mengineyo.

# SURA YA 5

## *KUNYONGA MISTARI NA MUKTADHA*

ꟷ

Nimeeleza baadhi ya mambo kuhusiana na historia ya Sura na milango ilivyowekwa kwenye Biblia. Hiyo ni hatua muhimu itakayokusaidia kuepuka KUNYOFOA mistari. Siku zingine wakati unasoma hebu "tambaa" kama vile hakuna Mistari na sura...kama unasoma Waraka kwa Waefeso usikimbilie WAEFESO 3:20 soma 1 hadi mwisho... utagundua ni kitabu kinachoeleweka sana. Au kama unasoma 1 Wakorintho usikimbilie sura ya 13 upendo upendo... hapana… _elewa MWANDISHI

alivyopanga hoja zake. Biblia haikuandikwa na WAHUNI ambao hawajui kupangilia mambo, na wewe usisome kihuni kwa kurukaruka kama "kangaroo". Hata uchambuzi wa vitabu vya Kiswahili Kidato cha Pili tulikuwa tunasoma kwanza kitabu chote baadaye tunaanza uchambuzi wa kitu kimoja baada ya kingine.

Even the Bible is the literature, why do we mishandle this sacred book?

Hebu fikiria ujinga tunaoupata kwa kusoma kitabu cha Ufunuo wa Yohana kwa sababu ya kuyabeba maandiko kizembe. Yaani mtu anaanza kutafuta madudu kule, mara 666, mara wanyama, mara papa, huku wanasiasa maarufu, Obama, Trump, Sijui China. yaani unasahau kuwa MWANDISHI ameanza kwa kusema HUU NO UFUNUO WA YESU KRISTO ALIOONYESHWA YOHANA... Yaani sura ya 1 na ya 2 watu wanapita kwa kasi ili kuwahi hao wanyama ambao hata hawaelewi.

Angalia ***Ufunuo wa Yohana 1:1***

***[1] Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi; naye akatuma kwa mkono wa malaika akamwonyesha mtumwa wake Yohana;***

Kitabu chote ni ufunuo wa Kristo ila kikianza kusomwa hakika unaona KRISTO AKIFUNIKWA na vitu vya

ajabu sana. Hii ni kwa sababu alama, ishara na lugha zilizopo kule kila mtu anajaribu kuzipa maana kwa kutumia kichwa chake.

Hivi ukisoma ramani ya Africa kujua maana ya alama zilizoko kwenye ramani hiyo unatoa kichwani mwako? Hapana. Ufunguo (key) upo hapo hapo kwenye ramani…

_

Imagine umesoma ***Wafilipi 4:13***

***[13] Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.***

Unaibuka nayo "NAYAWEZA MAMBO YOTE, NAWEZA BIASHARA, NAWEZA KUFAULU, NAWEZA .... NAWEZA... MAMBO LUKUKI......" Utagundua hauwezi mambo yote… _

wewe ni mhandisi huwezi udaktari, wewe ni mwanaume huwezi kubeba mimba, wala Mungu hakutii nguvu kuweza hayo. Hii utajua kuwa... HAYO MAMBO YOTE YAKO PALE PALE KWENYE HUO WARAKA… _

Angalia nyuma yake... ***Wafilipi 4:12-14***

***[12] Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote, na katika mambo yo yote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa.***

***[13] Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.***

***[14] Lakini mlifanya vema, mliposhiriki nami katika dhiki yangu***

Huyu ndugu anashukuru kwa sababu ya sadaka aliyopokea huku akionyesha anajua kuishi katika hali zote na Bwana amemwezesha kuwa hivyo... **KUDHILIWA NA KUFANIKIWA, KUSHIBA NA KUONA NJAA, KUWA NA VINGI NA KUPUNGUKIWA**.

Haya ndiyo mambo Paulo anasema anayaweza. Haya mambo hayamsukumi. FULL OR NILL HE IS STABLE IN THE LORD (Hii ndiyo maana ya kuridhika) ... Sasa unapokiri wakati unaingia kwenye chumba cha mtihani wa UE unamaanisha *unaweza kufeli na kufaulu?*

Kwa hiyo kusema Nayaweza mambo yote... jiulize yapi? Hayo hapo yametajwa.

Kwa hiyo...

Unaposoma maandiko KUBALI YA KWAMBA MAANA YA MAELEZO YA KILE MWANDISHI ANAONYESHA KIPO HUKO HUKO NDANI SIYO KICHWANI MWAKO.

BAKI NDANI KWANZA... ACHA BIBLIA IKUFUNDISHE, DO NOT TRUST YOU IMAGINATIONS THERE... TRUST SCRIPTURE

# SURA YA 6

## *LENGO KUU LA MAANDIKO MATAKATIFU*

Ukiangalia kwa makini jinsi Biblia ilivyopangwa unaweza kufikiri ni vitabu vingi vyenye taarifa nyingi kuhusu mambo mengi, lakini ukweli ni kwamba Biblia ni mkusanyiko wa maandiko, yaliyoandikwa na watu tofauti tofauti katika nyakati tofauti yakiwa na ujumbe mmoja nao ni UKOMBOZI WA MWANADAMU KWA NJIA YA YESU KRISTO a.k.a WOKOVU.

Hili ni jambo la muhimu sana. Maana ukianza kutumia Biblia kwa mambo mengine lazima ipwaye, maana siyo lengo lake. Ukiona ni kitabu cha kukusaidia kukuza uchumi wako ushapotea tayari maana kuna watu wengi wanakuza uchumi huku hawajui hata Mathayo ina sura ngapi, ukifikiri ni kitabu cha kufundishia urafiki, uchumba hadi ndoa unakuwa umeshaangukia pua, ukiona kama ni kitabu kinachofundisha kilimo unakuwa unashindana na Sokoine University of Agriculture... Narudia tena ujumbe ni Ukombozi wa Mwanadamu kwa njia ya Yesu Kristo. Sasa huu ujumbe siyo ujumbe mdogo kwa sababu watu wengi hawafundishwi vizuri hawauelewi wala hawana mzuka nao kabisa. Ni kama hadithi za kichovu kwa watu wengine, ndiyo maana wameamua kusaka mambo mengine kwenye Biblia.

Huo ujumbe umewasilishwa na waandishi wengi, wengi wao wakiwa hawajawahi kukutana… _

Sasa huu ujumbe umewasilishwa katika vitabu vya "Agano la Kale" yaani Mwanzo mpaka Malaki kama AHADI, Huku Waandishi wakitumia lugha, vitu, matukio na watu mbalimbali kuelezea AHADI HIYO YA MUNGU KUMKOMBOA MWANADAMU. Kwenye vitabu vya Mathayo mpaka Yohana ni udhihirisho wa mkombozi huyo katika mwili, Mathayo, Marko, Luka na Yohana wameandika uwepo wake

duniani miaka 33 na mambo aliyoyafanya na kusema kabla ya kutimiza huo ukombozi wa mwanadamu.

(Tutachambua kwa undani huko mbeleni). Eye witness or historical account.

Kitabu cha Matendo ya mitume ambacho kimeandikwa na Luka ikielezea kuanza kwa kazi ya kueneza hiyo habari ya ukombozi au Injili au habari njema kuwa sasa ile ahadi ya "Maandiko Matakatifu" imetimizwa.

Kwenye nyaraka za mitume kuanzia Waraka kwa Warumi ni maelezo kwa Waamini (walioipokea hiyo Injili) namna wanavyotakiwa kuenenda. Kwenye nyaraka maisha ya Mwamini yanawekwa wazi, kuhusu asili yao baada ya kupokea habari za ukombozi wao, namna ya kukua katika hilo na kuwaonyesha wengi nuru waliyoipokea. Ndiyo maana sehemu kubwa ya nyaraka waandishi wametumia lugha ya kawaida zaidi... hakuna mafumbo, Mithali, nahau, kama Vitabu vingine.

Sasa hebu turudi kuangalia **lengo kuu la maandiko matakatifu… _**

Kwa hiyo, Mafarisayo na Masadukayo walisoma vitabu vile vile lakini waliingia chaka kwa sababu walikuwa HAWAMWONI HUKO YESU KRISTO SHUJAA WA UZIMA.

Wao walikuwa wanasoma kutafuta mambo mengine mengi ikiwa ni pamoja na UZIMA.

Yesu anawaambia kwenye ***Yohana 5:39-40***

***[39] Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia.***

***[40] Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima.***

Hii ni sawa na kusema wangesoma vizuri na kwa umakini Mwanzo mpaka Malaki wangemwona "mtu" Yesu kutokea kule na kwamba ingekuwa rahisi wao kumwona MWENYE UZIMA.

Angalia namna Filipo alipomwelezea Yesu kwa Nathanieli....

***Yohana 1:45***

***[45] Filipo akamwona Nathanaeli, akamwambia, Tumemwona yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii, Yesu, mwana wa Yusufu, mtu wa Nazareti.***

Filipo anakiri kitu cha ajabu sana... **Musa katika torati pamoja na manabii wameandika habari za Yesu**. woow...

Yesu alipowatokea Kleopa na mwenzake aliwaeleza habari zake kwa kutumia maandiko matakatifu.

***Luka 24:26-27***

[26] Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?

***[27] Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.***

Angalia hili.... **AKAANZA KUTOKA MUSA NA MANABII WOTE**, Siyo Musa na baadhi ya Manabii, bali manabii **WOTE** kwa hiyo **MANABII WOTE** walitabiri habari za Yesu.

Yesu alipokwenda kuongea na wanafunzi wake wengine alisisitiza jambo lile lile kwamba KUPATA MATESO, KUFA NA KUFUFUKA imeandikwa kwenye vitabu vya **Musa, Zaburi na manabii.**

Angalia ***Luka 24:44-47***

***[44] Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.***

***[45] Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko.***

***[46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;***

***[47] na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.***

Ukisikia Musa ujue ni vitabu vya kwanza VITANO... yaani Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu na Kumbukumbu la Torati.

Angalia jinsi Petro anavyoweka...

***Matendo ya Mitume 3:18***

***[18] Lakini mambo yale aliyohubiri Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake wote, ya kwamba Kristo wake atateswa, ameyatimiza hivyo.***

Manabii wote wamehubiri ujumbe wa Injili.

Huwa unaona Injili kwa akina Isaya au unaona laana za ukoo na vifungo, namna ya kumuua adui yako? Unasoma Zaburi ili Mungu awaaibishe adui zako?

Petro anaongeza kusema…

***Matendo ya Mitume 3:24***

***[24] Naam, na manabii wote tangu Samweli na wale waliokuja baada yake, wote walionena, walihubiri habari za siku hizi.***

Siku gani? Za Kristo KUTESWA, Kufa na kufufuka....

# SURA YA 7

## *UNASOMA KAMA YESU AU FARISAYO?*

Namna Bwana wetu Yesu Kristo alivyosoma maandiko matakatifu (au vitabu vya Agano la Kale) ni tofauti na Mafarisayo na Masadukayo

kwa sehemu kubwa sana ni tofauti pia na namna ya watu wengi leo. Unajua tunaweza tukawa tunawacheka Mafarisayo lakini sisi tukawa tumekubuhu kuliko wao. Yaani unahisi wewe unapatia huku unakosea. Hii inatutokea kwa sababu tulipewa maandiko bila kuelekezwa namna ya kutumia kwa hiyo tunafanya ili mradi au kwa kufuata mawazo yetu.

Mafarisayo na Masadukayo ni watu waliokuwa "deep" kwa habari ya kujua maandiko pengine kuliko wengi wetu leo. Nikisema kujua simaanishi walikuwa na tafsiri sahihi. Mtu mpaka aitwe Rabi si lelemama, uwe na uhakika anaweza kukariri maandiko kwa sehemu kubwa.

Kukariri na kujaza maandiko mengi kichwani siyo mbaya kabisa ni kongole, ni heko, ni jambo jema... ishu iko kwenye KUTAFSIRI (INTERPRETATION).

Naomba uelewe hili Leo na usisahau **MAANDIKO MATAKATIFU SIYO MAMBO YA KUNUKUU TU, BALI YANATAKIWA KUTAFSIRIWA KABLA YA KUTUMIA**. *(INTERPRET BEFORE YOU APPLY).*

Ukisoma Zaburi

***Zaburi 8:4***

***[4] Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, Na binadamu hata umwangalie?***

Ukishasoma halafu unaanza kusema "MUNGU ANASEMA MTU SI KITU, NA MANENO MENGINE MENGI" angalau utulie ujue ni nini kinazungumziwa, mtu gani? Alifanya nini? Wapi?

So don't rush to application.

Imagine unasoma Zaburi ya 35 kwa sababu tu kuna watu unawaona ni adui unaanza kunukuu...

***Zaburi 35:1-6***

***[1] Ee BWANA, utete nao wanaoteta nami, Upigane nao wanaopigana nami.***

***[2] Uishike ngao na kigao, Usimame unisaidie.***

***[3] Uutoe na mkuki uwapinge wanaonifuatia, Uiambie nafsi yangu, Mimi ni wokovu wako.***

***[4] Waaibishwe, wafedheheshwe, Wanaoitafuta nafsi yangu. Warudishwe nyuma, wafadhaishwe, Wanaonizulia mabaya.***

***[5] Wawe kama makapi mbele ya upepo, Malaika wa BWANA akiwaangusha chini.***

***[6] Njia yao na iwe giza na utelezi, Malaika wa BWANA akiwafuatia.***

Relax, Tulia, Tafakari...

MWANDISHI alikuwa anamaanisha nini?

KINYUME na hapo ndugu yangu unaweza ukawa unakosa lengo la maandiko

matakatifu kila mara usomapo.

**Sasa tuangalie Yesu alivyosoma maandiko matakatifu!**

YESU ALISOMA MAANDIKO KAMA KITABU KINACHOMHUSU YEYE... YAANI MWANZO MPAKA MALAKI YEYE NDIYO **CENTRAL FIGURE.**

Yes, Yesu alisoma kama kitabu KINACHOMHUSU Yeye. Ukisoma kivingine utapata dini za kutosha kabisa na mafunuo ya ajabu ajabu.

Imagine dini ya kiyahudi ni matokeo ya watu wanaosoma maandiko hayo kama Musa ndiyo CENTRAL FIGURE... Mafarisayo na Masadukayo pia wanasoma lakini Yesu siyo kiini kwenye mioyo yao...

Cha ajabu leo wengine wanasoma kwa jicho la Uchumi kila kitu kinavurugika, wengine kwa jicho la siku za mwisho huko watakutana na vituko vya kubashiri Kurudi kwa Kristo, New World Order, watu wanaanza kuishi kwa speculation na assumptions mwishoni wanakuja kuwa disappointed kama akina KIBWETERE... wengine

wanaangalia kwa jicho la Uongozi mpaka Yesu anaacha kuonekana kama MWOKOZI ila just a leader, wengine wanaangalia kama kitu cha kupambana na maadui mpaka wakristo wanaanza kuishi kama WACHAWI, utashangaa nikikuambia mambo mengi zaidi ya hayo..

Ukristo wa KWELI unapatikana tu kama utasoma maandiko ya Agano la Kale kwa jicho la Kristo.

Yes, Kristo. Yes, mitume walifundisha habari za Yesu Kristo na WOKOVU kutokea Agano la Kale.

Ndiyo maana Yesu alikuwa akichukua Maandiko anasoma kwa mamlaka kamili mpaka wanamshangaa.

***Luka 4:17-22***

***[17] Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palipoandikwa,***

***[18] Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa,***

***[19] Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.***

***[20] Akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, akaketi; na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho.***

***[21] Akaanza kuwaambia, Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu.***

***[22] Wakamshuhudia wote, wakiyastaajabia maneno ya neema yaliyotoka kinywani mwake, wakasema, Huyu siye mwana wa Yusufu?***

Watu walishangaa kwa sababu hawakutegemea mtu yeyote awe na ujasiri wa kusema Maneno yale...

**Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu**

Kwa hiyo utimilifu wa maandiko ni Yesu... yaani ahadi zote unazoziona kule

zinatimia ndani ya Yesu Kristo.

Huko tulipotoka tulisema, kwa lugha mbalimbali zilzotumika na mambo yanayoonekana kuwa mengi zote kwa pamoja ni ahadi ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu.

Ndiyo maana Yesu akawaambia...

***Yohana 5:39-40***

***[39] Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia.***

***[40] Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima.***

Kwa hiyo maandiko YANATAKIWA kukuleta kwa Kristo, Maandiko yanamfunua Kristo na YANATAKIWA kusomwa hivyo, siyo kitabu cha kuwafunua maadui zao, siku za mwisho, habari za vita, Do's and Don'ts ni Kristo ameandikiwa huko.

Angalia alichowaambiwa kuhusu Maneno ya Musa...

***Yohana 5:45-47***

***[45] Msidhani kwamba mimi nitawashitaki kwa Baba; yuko anayewashitaki, ndiye Musa, mnayemtumaini ninyi.***

***[46] Kwa maana kama mngalimwamini Musa, mngeniamini mimi; kwa sababu yeye aliandika habari zangu.***

***[47] Lakini msipoyaamini maandiko yake, mtayaamini wapi maneno yangu?***

Kwa hiyo Musa aliandika kabisa habari za Yesu na alishangaa kwamba wanajionyesha kwamba wanamkubali Musa kumbe hata ujumbe ambao Musa aliuandika hawakuuelewa hata kidogo.

HII INA MAANA UKITULIA NA UKAMSOMA MUSA VIZURI UTAMWONA KRISTO WAZI KABISA (Tutapita huko).

Twendeni Taratibu tutafika.

HATUNA HARAKA...

UKIWEZA RUDIA TENA KUSOMA KUANZIA SEHEMU YA KWANZA!.

# SURA YA 8

***ILI LITIMIE NENO LILILONENWA***

Kuna lugha ambazo unaweza kuona zimeenea sana katika Vitabu Vinne vya Injili vitabu vinavyozungumzia "Maisha ya Yesu, KUZALIWA, huduma yake katika mwili, kufa na kufufuka kwake"

Ni Maneno yanayotuhakikishia kuwa maandiko matakatifu yaliandikwa macho yote yakiwa kwake. Musa aliandika akiwa na anamtazama Yeye, Manabii walitabiri wakimwona Yeye.

Angalia baadhi ya Maneno hayo. **ILI LITIMIE NENO AU ANDIKO AU YALIYOANDIKWA AU KUWATIMIZIA AHADI**

Sehemu ziko nyingi ila tutatumia chache tu kwa ajili ya kutupa mwanga.

Ukifuatilia vizuri Maneno haya utagundua ni habari za mambo aliyoyasema na kuyafanya Yesu Kristo kwa lengo la kutimiza unabii au maandiko yaliyoandikwa kwa habari zake.

***Mathayo 1:21-23***

***[21] Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.***

***[22] Hayo yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema,***

***[23] Tazama, bikira atachukua mimba, Naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake Imanueli; Yaani, Mungu pamoja nasi***

Haya maneno ambayo malaika aliyesema kwa Yusufu katika ndoto na hakuyaokota mtaani bali kwenye maandiko… _

Angalia ***Isaya 7:14***

***[14] Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli.***

Ukitazama kwa makini kitu pekee ambacho malaika ameongeza ni tafsiri ya Imanueli yaani Mungu pamoja nasi.

Hata kisa cha Yesu kupanda mwana punda na yenyewe ilikuwa "documented"

***Mathayo 21:4-5***

***[4] Haya yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema,***

***[5] Mwambieni binti Sayuni Tazama, mfalme wako anakuja kwako, Mpole, naye amepanda punda, Na mwana-punda, mtoto wa punda.***

Hiki kisa kilikuwa recorded katika unabii wa Zekaria ...

Angalia ***Zekaria 9:9***

***[9] Furahi sana, Ee binti Sayuni; Piga kelele, Ee binti Yerusalemu; Tazama, mfalme wako anakuja kwako; Ni mwenye haki, naye ana wokovu; Ni mnyenyekevu, amepanda punda, Naam, mwana punda, mtoto wa punda.***

Walipopigia kura Mavazi yake...

***Yohana 19:24***

***[24] Basi wakaambiana, Tusiipasue, lakini tuipigie kura, iwe ya nani. Ili litimie andiko lile linenalo, Waligawanya nguo zangu, Na vazi langu wakalipigia kura. Basi ndivyo walivyofanya wale askari.***

Haya Maneno utayaona kwenye…

***Zaburi 22:18***

***[18] Wanagawanya nguo zangu, Na vazi langu wanalipigia kura.***

Ukiangalia kwa haraka utafikiri Daudi alikuwa anazungumzia Mavazi yako lakini alikuwa ana "dramatize" nafasi ya Yesu akiwa anatoa unabii.

Unaweza ukafikiri Daudi alivuliwa nguo na kupigiwa kura.

Maandiko hayamhusu Daudi ila Daudi mwenyewe alimzungumzia habari za Kristo katika uandishi wake au unabii wake.

Angalia sehemu nyingine Daudi alichofanya...

Angalia jinsi Petro alivyochambua unabii wa Daudi...

***Matendo ya Mitume 2:22,25-36***

***[22] Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya: Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua;***

***[25] Maana Daudi ataja habari zake, Nalimwona Bwana mbele yangu siku zote, Kwa kuwa yuko upande wa mkono wangu wa kuume, nisitikisike.***

***[26] Kwa hiyo moyo wangu ukapendezewa, ulimi wangu ukafurahi; Tena mwili wangu nao utakaa katika matumaini.***

***[27] Kwa maana hutaiacha roho yangu katika kuzimu; Wala hutamtoa Mtakatifu wako aone uharibifu.***

***[28] Umenijuvisha njia za uzima; Utanijaza furaha kwa uso wako.***

***[29] Waume, ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo.***

***[30] Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi;***

***[31] yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu.***

***[32] Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake.***

***[33] Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia.***

***[34] Maana Daudi hakupanda mbinguni; bali yeye mwenyewe anasema, Bwana alimwambia Bwana wangu, Keti upande wa mkono wangu wa kuume.***

***[35] Hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako.***

***[36] Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo.***

Kuanzia mstari wa 29 unaona Petro anaeleza kuwa Daudi alikuwa hazungumzii habari zake hata kidogo ila habari za Yesu Kristo.

Daudi hakuwa anazungumzia yeye kutoachwa kwenye mauti (kufufuliwa) ila ukiangalia kizembe unaweza kufikiri Daudi alikuwa anajizungumzia yeye.

CHANGAMOTO NI KWAMBA MARA NYINGI TUNATUMIA ZABURI BILA KUTAFSIRI...

Kwa habari ya Daudi, Paulo pia aliandika akizungumzia kutoka kwenye Zaburi ya 2.

***Matendo ya Mitume 13:29-37***

***[29] Hata walipokwisha kumaliza yote aliyoandikiwa, wakamtelemsha katika ule mti, wakamweka kaburini.***

***[30] Lakini Mungu akamfufua katika wafu;***

***[31] akaonekana siku nyingi na wale waliopanda naye kutoka Galilaya hata Yerusalemu, ambao sasa ndio walio mashahidi wake mbele ya watu.***

***[32] Na sisi tunawahubiri habari njema ya ahadi ile waliyopewa mababa,***

***[33] ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu ahadi hiyo, kwa kumfufua Yesu; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili, Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa.***

***[34] Tena ya kuwa alimfufua katika wafu, asipate kurudia uharibifu, amenena hivi, Nitawapa ninyi mambo matakatifu ya Daudi yaliyo amini.***

***[35] Kwa hiyo anena na pengine, Hutamwachia Mtakatifu wako kuona uharibifu.***

***[36] Kwa maana Daudi, akiisha kulitumikia shauri la Mungu katika kizazi chake, alilala, akawekwa pamoja na baba zake, akaona uharibifu.***

***[37] Bali huyu aliyefufuliwa na Mungu hakuona uharibifu.***

Angalia hili... ***Luka 24:25-27,44-47***

***[25] Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii!***

***[26] Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?***

***[27] Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.***

***[44] Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.***

***[45] Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko.***

***[46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;***

***[47] na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.***

Yaani tunaona inamhusu Daudi au sisi wenyewe.

Wewe huwa unatumiaje Zaburi?

Unasoma kwa jicho lipi?

La Daudi?

La maadui zako?

La mahitaji yako?

Au la KRISTO?

Je unamwaona KRISTO kwenye maandiko?

Kiini cha Vitabu vya Musa, Manabii na Zaburi ni Yesu Kristo.

Ukiona vyote ukakosa kuona hayo. UMEPOTEA MCHANA.

# SURA YA 9

## *KUYAHUBIRI KAMA YALIVYOTIMIA: PETRO*

Tuyaangalie tena mambo yaliyotimizwa katika maandiko ili tujifunze namna ya kuelekeza macho yetu kwa Kristo na kazi yake kubwa ya ukombozi wa mwanadamu.

Tuanze kwa Maneno ya Petro.

Baada ya Petro na Yohana kumnyanyua yule kiwete watu wakakusanyika... Tofauti na wahubiri wengi leo, badala ya Petro kuwaelekeza watu juu ya ule muujiza

akaanza kuhubiri habari za Kristo kutoka kwenye maandiko...

Angalia shule yake ya UINJILISTI...

***Matendo ya Mitume 3:17-26***

***[17] Basi sasa, ndugu, najua ya kuwa mliyatenda haya kwa kutokujua kwenu, kama na wakuu wenu walivyotenda.***

***[18] Lakini mambo yale aliyohubiri Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake wote, ya kwamba Kristo wake atateswa, ameyatimiza hivyo.***

***[19] Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana;***

***[20] apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani;***

***[21] ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu.***

***[22] Kwa maana Musa kweli alisema ya kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi.***

***[23] Na itakuwa ya kwamba kila mtu asiyemsikiliza nabii huyo ataangamizwa na kutengwa na watu wake.***

***[24] Naam, na manabii wote tangu Samweli na wale waliokuja baada yake, wote walionena, walihubiri habari za siku hizi.***

***[25] Ninyi mmekuwa watoto wa manabii na wa maagano yale, ambayo Mungu aliagana na baba zenu, akimwambia Ibrahimu, Katika uzao wako kabila zote za ulimwengu zitabarikiwa.***

***[26] Mungu, akiisha kumfufua mtumishi wake Yesu, alimtuma kwenu ninyi kwanza, ili kuwabarikia kwa kumwepusha kila mmoja wenu na maovu yake.***

Anaanza kwa kusema MUNGU ALIHUBIRI ZAMANI KWA VINYWA VYA MANABII WAKE WOTE KWAMBA KRISTO ATATESWA. na imetimia.

Anaendelea kuonyesha baadhi ya sehemu habari hiyo imetajwa.

Akaanza na Musa... Je, Musa alisema hayo wapi?

Angalia ***Kumbukumbu la Torati 18:15,18-19***

***[15] BWANA, Mungu wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye.***

***[18] Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru.***

***[19] Hata itakuwa, mtu asiyesikiliza maneno yangu atakayosema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake.***

Ukiendelea kutazama Petro anaonyesha kuwa asiyemsikiliza nabii huyo ataangamizwa. Anaangamizwaje?

Hii iko wazi. kutomsikiliza ni KUTOMWAMINI na KUANGAMIZWA NI KUPOTEA/KUHUKUMIWA KWA SABABU YA KUTOMWAMINI

***Yohana 3:16-18***

***[16] Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.***

***[17] Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye.***

***[18] Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.***

Manabii wote tangu Samweli walikuwa na ujumbe mmoja. wa IMANI KATIKA KAZI YA KRISTO YESU YAANI KUFA NA KUFUFUKA NA MATOKEO YAKE KWETU

Ndiyo maana Samweli ANATAJWA kwenye "Hall of Faith"

***Waebrania 11:32***

***[32] Nami niseme nini tena? Maana wakati usingenitosha kuleta habari za Gideoni na Baraka na Samsoni na Yeftha na Daudi na Samweli na za manabii;***

Hii inamaana Samweli alihubiri habari za Kristo kama Unabii... kwenye nafasi yake kama nabii... Petro anasema **WALIHUBIRI HABARI ZA SIKU HIZI**

**Siku hizi ni siku za UFUFUO wa Yesu.**

Petro anataja pia ahadi aliyopewa Ibrahimu kwamba katika uzao wake kabila zote za ulimwengu zitabarikiwa.

Swali ambalo linatakiwa kuja kichwani kwako ni ... aliahidiwa wapi? Ahadi ile ilikuwa na maana gani? Uzao huo ni upi na baraka hizo ni zipi?

Kwa nini Petro ahusishe ufufuo wa Yesu na baraka kwa kabila zote za ulimwengu?

Ibrahimu alipokwenda kumtoa Isaka malaika alimtokea na kumweleza mambo kadhaa.

***Mwanzo 22:15-18***

***[15] Malaika wa BWANA akamwita Ibrahimu mara ya pili kutoka mbinguni***

***[16] akasema, Nimeapa kwa nafsi yangu asema BWANA, kwa kuwa umetenda neno hili, wala hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee,***

***[17] katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao;***

***[18] na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa sababu umetii sauti yangu.***

Huu uzao ni Isaka? La hasha! Ulikuwa ni unabii wa Kristo,

angalia ***Wagalatia 3:16***

***[16] Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi, Kwa wazao, kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, Kwa mzao wako, yaani, Kristo.***

Uzao uliokuwa unazidishwa ni uzao wa Kristo na kuzidishwa huko ni kanisa.

Angalia... ***Wagalatia 3:26-29***

***[26] Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu.***

***[27] Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.***

***[28] Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu.***

***[29] Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.***

Kwa hiyo uzao wa Ibrahimu umekuwa kama nyota za mbinguni kwa sababu umeongezeka katika Kristo yaani WOTE WALIOAMINI KATIKA KRISTO WAMEMVAA KRISTO NA HIVYO WOTE NI UZAO WA IBRAHIMU.

Je, wanakuwaje uzao wa Ibrahimu? Kwa kumpokea Roho ndani yao. Na hii ndiyo ahadi aliyopewa Ibrahim siyo utajiri kama wengi wanavyohubiri kwa nguvu.

Angalia ***Wagalatia 3:13-14***

***[13] Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti;***

***[14] ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani.***

Ahadi ni ROHO KWA NJIA YA IMANI au KUAMINI.

Kila amwaminiye Yesu anapokea Roho, anafanya mwana wa Mungu au uzao wa Ibrahim kwa uzidisho... Uzao KRISTO... Uzao WANAOBATIZWA KATIKA KRISTO (WAAMINI).

# SURA YA 10

## *KUYAHUBIRI KAMA YALIVYOTIMIA: PAULO*

Kuna Baada ya kuangalia jinsi Petro alivyomfunua Kristo katika maandiko hebu tuangalie MAHUBIRI YA PAULO katika SINAGOGI alipopewa nafasi ya kuhubiri na jinsi alivyotumia vizuri maandiko ya Agano la Kale kumfunua KRISTO.

Matendo ya mitume 13:16-41

Twende hatua kwa hatua.

***Matendo ya Mitume 13:14-15***

***[14] Lakini wao wakatoka Perge, wakapita kati ya nchi, wakafika Antiokia, mji wa Pisidia, wakaingia katika sinagogi siku ya sabato, wakaketi.***

***[15] Kisha, baada ya kusomwa torati na chuo cha manabii, wakuu wa sinagogi wakatuma mtu kwao, na kuwaambia, Ndugu, kama mkiwa na neno la kuwafaa watu hawa, lisemeni.***

Hapa mtume Paulo anakaribishwa atoe hotuba yake baada ya Torati na Manabii kusomwa.

ANGALIA SASA NENO LA KUWAFAA WATU KULINGANA NA PAULO.

***Matendo ya Mitume 13:16-23***

***[16] Paulo akasimama, akawapungia mkono, akasema, Enyi waume wa Israeli, nanyi mnaomcha Mungu, sikilizeni.***

***[17] Mungu wa watu hawa Israeli aliwachagua baba zetu, akawatukuza watu hao, walipokuwa wakikaa kama wageni katika nchi ya Misri, na kwa mkono ulioinuliwa akawatoa, akawaongoza.***

***[18] Na kwa muda wa miaka kama arobaini akawavumilia katika jangwa.***

***[19] Na alipokwisha kuwaharibu mataifa saba katika nchi ya Kanaani akawapa nchi yao iwe urithi kwa muda wa miaka kama mia nne na hamsini;***

***[20] baada ya hayo akawapa waamuzi hata zamani za nabii Samweli.***

***[21] Hatimaye wakaomba kupewa mfalme; Mungu akawapa Sauli mwana wa Kishi, mtu wa kabila ya Benyamini, kwa muda wa miaka arobaini.***

***[22] Na alipokwisha kumwondoa huyo, akamwinua Daudi awe mfalme wao ambaye alimshuhudia, akisema, Nimemwona Daudi, mwana wa Yese, mtu anayeupendeza moyo wangu, atakayefanya mapenzi yangu yote.***

***[23] Katika uzao wake mtu huyo Mungu amewaletea Israeli Mwokozi, yaani, Yesu, kama alivyoahidi***

Paulo ALICHOKIFANYA hapa ni kuweka SUMMARY ya Matukio mengi sana... hadi kwenye ahadi ya Mungu kumwinulia Daudi mfalme atakayetawala milele. Uwe na uhakika kuna watu wengi walikuwa wanafikiri ahadi hiyo ni Sulemani (Solomon)...

Alianza kwenye vitabu vya Musa yaani Kutoka mpaka Wafalme...

Ahadi kwa Daudi kwamba uzao wake utatawala milele haukuwa juu ya Sulemani kwani Sulemani hakutawala milele ila nafasi yake ilikuwa ni lugha ya picha kuelezea kile kilicho cha milele yaani Kristo.

Angalia ahadi ilipoanzia ***1 Samweli 13:13-14***

***[13] Naye Samweli akamwambia Sauli, Umefanya upumbavu; hukuishika amri ya BWANA, Mungu wako, aliyokuamuru; kwa maana BWANA angaliufanya ufalme wako kuwa imara juu ya Israeli milele.***

***[14] Lakini sasa ufalme wako hautadumu; BWANA amejitafutia mtu aupendezaye moyo wake, naye BWANA amemwamuru yeye kuwa mkuu juu ya watu wake, kwa sababu wewe hukulishika neno lile BWANA alilokuamuru.***

Kwa habari ya Daudi wazao (uzao) wake...

***Zaburi 89:20-21, 28-29***

***[20] Nimemwona Daudi, mtumishi wangu, Nimempaka mafuta yangu matakatifu.***

***[21] Ambaye mkono wangu utakuwa thabiti kwake, Na mkono wangu utamtia nguvu.***

***[28] Hata milele nitamwekea fadhili zangu, Na agano langu litafanyika amini kwake.***

***[29] Wazao wake nao nitawadumisha milele, Na kiti chake cha enzi kama siku za mbingu.***

Hii ahadi siyo ufalme wa kikawaida. ufalme wa milele, ahadi ya milele ni zaidi ya nafasi ya kiuongozi katika siasa ni ufalme unaodumu milele ni UFALME WA KRISTO.

Tuendelee na ***Matendo ya Mitume 13:24-25***

***[24] Yohana alipokuwa amekwisha kuwahubiri watu wote wa Israeli habari za ubatizo wa toba, kabla ya kuja kwake.***

***[25] Naye Yohana alipokuwa akimaliza mwendo wake alinena, Mwanidhani mimi kuwa nani? Mimi siye. Lakini, angalieni, anakuja mmoja nyuma yangu ambaye mimi sistahili kumlegezea viatu vya miguu yake.***

Ghafla Paulo anarukia kuelezea habari za Yohana Mbatizaji alivyothibitisha kuwa Mfalme huyo aliyetabiriwa ni Kristo na anasimama kama nabii wa mwisho aliyetabiri na kumwona MWOKOZI.

***Matendo ya Mitume 13:26-34***

***[26] Ndugu zangu, wana wa ukoo wa Ibrahimu, na hao miongoni mwenu wanaomcha Mungu, kwetu sisi neno la wokovu huu limepelekwa.***

***[27] Kwa maana wakaao Yerusalemu, na wakuu wao, kwa kuwa hawakumjua yeye, wala maneno ya manabii yanayosomwa kila sabato, wameyatimiza kwa kumhukumu.***

***[28] Na ijapokuwa hawakuona sababu ya kumfisha wakamwomba Pilato auawe.***

***[29] Hata walipokwisha kumaliza yote aliyoandikiwa, wakamtelemsha katika ule mti, wakamweka kaburini.***

***[30] Lakini Mungu akamfufua katika wafu;***

***[31] akaonekana siku nyingi na wale waliopanda naye kutoka Galilaya hata Yerusalemu, ambao sasa ndio walio mashahidi wake mbele ya watu.***

***[32] Na sisi tunawahubiri habari njema ya ahadi ile waliyopewa mababa,***

***[33] ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu ahadi hiyo, kwa kumfufua Yesu; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili, Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa.***

***[34] Tena ya kuwa alimfufua katika wafu, asipate kurudia uharibifu, amenena hivi, Nitawapa ninyi mambo matakatifu ya Daudi yaliyo amini.***

Paulo anawakumbusha mambo ambayo yalikuwa yanasomwa kila sabato (Mwanzo mpaka Malaki) ni

habari za Yesu. Ni unabii, ni ahadi... na kuwa Mungu alipanga kutimiza.

Na wao bila kujua wakayatimiza hizo ahadi kwa kumhukumu na kumsulubisha kisha Mungu akamfufua kutoka wafu... kule kumfufua kutoka wafu ndiyo ahadi ambayo Mungu akiwapa mababa (wazee wa Israel kwenye maandiko).

UFUFUO wa Yesu Kristo ndiyo habari njema walizopewa wazee hao... na baada ya hapo akanukuu sehemu nyingine ambapo ahadi ya kumfufua Yesu imetajwa kwenye Zaburi ya pili...

***Zaburi 2:7***

***[7] Nitaihubiri amri; BWANA aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa.***

Hiyo kusema Mambo matakatifu ya Daudi yaliyo imara (UFUFUO) ni ku paraphrase Isaya 55:3

***Isaya 55:3***

***[3] Tegeni masikio yenu, na kunijia; Sikieni, na nafsi zenu zitaishi; Nami nitafanya nanyi agano la milele, Naam, rehema za Daudi zilizo imara.***

Yaani imara kwa sababu ya udhabiti wake, hataona MAUTI tena na kazi ya Ukombozi hukamilika katika UFUFUO.

Huu ni unabii aliopewa Daudi kwenye ***2 Samweli 7:12-13***

***[12] Nawe siku zako zitakapotimia, ukalala na baba zako, nitainua mzao wako nyuma yako, atakayetoka viunoni mwako, nami nitaufanya imara ufalme wake.***

***[13] Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu, nacho kiti cha enzi cha ufalme wake nitakifanya imara milele.***

Hii nyumba atakayojenga Kristo ni kanisa la Mungu au mwili wa Kristo (tutajadili huko mbele) ... Sulemani alifanya kama unabii pia kwa kujenga hakalu.

Tuendelee na ***Matendo ya Mitume 13:35-37***

***[35] Kwa hiyo anena na pengine, Hutamwachia Mtakatifu wako kuona uharibifu.***

***[36] Kwa maana Daudi, akiisha kulitumikia shauri la Mungu katika kizazi chake, alilala, akawekwa pamoja na baba zake, akaona uharibifu.***

***[37] Bali huyu aliyefufuliwa na Mungu hakuona uharibifu.***

Hii ya Daudi kuimba katika ***Zaburi 16:10***

***[10] Maana hutakuachia kuzimu nafsi yangu, Wala hutamtoa mtakatifu wako aone uharibifu.***

Hakuwa anajizungumzia yeye kwa kuwa iko wazi ya kuwa alimaliza kusudi lake kisha akafa ila yafaa kujua kuwa alikuwa haneni habari zake isipokuwa za Kristo kutobaki kwenye uharibifu ila ATAFUFULIWA.

Paulo anaonyesha lengo la Kristo kufufuka katika…

***Matendo ya Mitume 13:38-39***

***[38] Basi, na ijulikane kwenu, ndugu zangu, ya kuwa kwa huyo mnahubiriwa msamaha wa dhambi;***

***[39] na kwa yeye kila amwaminiye huhesabiwa haki katika mambo yale yote asiyoweza kuhesabiwa haki kwa torati ya Musa.***

Yesu Kristo kwa kufufuka kwake ni uhakika kuwa Msamaha wa dhambi unatakiwa kuhubiriwa. Cha ajabu ni kwamba hajasema MNAOMBA MSAMAHA WA DHAMBI. ILA MAHUBIRI YANATAKIWA YAWE **"JAMANI MMESAMEHEWA DHAMBI ZENU"**

Sasa, yale ambayo walikuwa wanajitahidi kujitakasa kwa sheria ya Musa sasa inahubiriwa kwamba MSAMAHA UNAPATIKANA BURE... Na yule anayeamini ndiye anayepokea... na hapo anakuwa AMEHESABIWA HAKI.

Paulo hakuishia tu hapo... kwenye hiyo hiyo ***Matendo ya Mitume 13:40-41***

***[40] Angalieni, basi, isiwajilie habari ile iliyonenwa katika manabii.***

***[41] Tazameni, enyi mnaodharau, kastaajabuni, mkatoweke; kwa kuwa natenda kazi mimi siku zenu, kazi ambayo msingeisadiki kabisa, ijapo mtu akiwasimulia sana.***

Hii kuonyesha kwamba unabii haukutabiri tu matokeo ya kuamini UFUFUO wa Yesu Kristo uletao Msamaha wa dhambi ila pia hatari kwa wale watakaoukataa ujumbe huo wa Msamaha kwa kufufuka kwake.

Haya ni Maneno ambayo nabii Habakuki aliyasema kwenye ***Habakuki 1:5***

***[5] Angalieni, enyi mlio kati ya mataifa, katazameni, kastaajabuni sana; kwa maana mimi natenda tendo siku zenu, ambalo hamtaliamini hata mkiambiwa.***

Na hii ndiyo shida ya watu hata Leo... unakomaa kumweleza mtu juu ya Msamaha bure wa Mungu kwa kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo lakini bado anakomaa kutafuta huo Msamaha badala ya KUPOKEA kwa imani na kumshukuru Mungu tena ukionekana unakomaa kusema Mungu anawapenda na wale hawahukumu watu wanakunja ndita na hasira juu. Na watu hawa nao wanaitwa wakristo kabisa ila ukweli ni kwamba siyo

WAAMINI kwa sababu hawaamini kwamba wamepewa Msamaha wa dhambi. Ni jambo la kustaajabisha.

Luka aliandika katika ***Luka 24:44-47***

***[44] Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.***

***[45] Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko.***

***[46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;***

***[47] na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.***

Kwa hiyo kuamini UFUFUO wa Yesu Kristo ni kuamini ya kuwa kwa KUTESWA, na kufufuka kwake wewe umepata Ondoleo (msamaha) wa dhambi. Ndiyo maana hata iweje mtu anayeamini (Mwamini) hawezi kuitwa mwenye dhambi kwa sababu dhambi zake zimeondolewa.

Hii haina maana hatafanya kosa lolote (maandiko hayatetei watu kufanya maovu) lakini *ikitokea* amefanya Mungu hamhesabii kuwa kuwa na dhambi.

Haya mambo Daudi huyo huyo alitabiri wazi ***Warumi 4:6-8***

***[6] Kama vile Daudi aunenavyo uheri wake mtu yule ambaye Mungu amhesabia kuwa na haki pasipo matendo,***

***[7] Heri waliosamehewa makosa yao, Na waliositiriwa dhambi zao.***

***[8] Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi.***

Haya Daudi aliyasema kwenye ***Zaburi 32:1-2***

***[1] Heri aliyesamehewa dhambi, Na kusitiriwa makosa yake.***

***[2] Heri BWANA asiyemhesabia upotovu, Ambaye rohoni mwake hamna hila.***

Ni kiburi cha hali ya juu KUJIHESABIA DHAMBI WAKATI MUNGU HAKUHESABII...

Ikiwa unaamini katika hili, UNAYO HERI. UMEBARIKIWA. Na wale wasioamini dhambi zao zinakaa. Maana kwa jitihada zao hawataweza hata siku moja kumpendeza Mungu.

Tena Paulo anasema katika ***Warumi 10:1-4***

***[1] Ndugu zangu, nitakayo sana moyoni mwangu, na dua yangu nimwombayo Mungu, ni kwa ajili yao, ili waokolewe.***

***[2] Kwa maana nawashuhudia kwamba wana juhudi kwa ajili ya Mungu, lakini si katika maarifa.***

***[3] Kwa maana, wakiwa hawaijui haki ya Mungu, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu.***

***[4] Kwa maana Kristo ni mwisho wa sheria, ili kila aaminiye ahesabiwe haki.***

HAKI HUPATIKANA KWA IMANI (KUAMINI KAZI YA MSALABA) NA SIYO KWA MATENDO YAKO.

# SURA YA 11

## *UBAKI UKIMWONA MWANA PEKEE*

Kuna Baada ya kumtazama Petro na Paulo walivyotafsri Ahadi ya Mungu ya ukombozi katika maandiko (Agano la Kale) sasa tuangalie baadhi ya vitu vitakavyokusaidia uone kama wao walivyyoona na kutafsiri.

Naomba uelewe hili: Ule mgawanyo wa vitabu kwenye Biblia yako kuwa huku ni Agano Jipya na huku ni Agano la Kale umefanya watu wengi waone kama ni vitabu viwili tofauti.

Ujumbe wa Biblia ni mmoja kutokea Mwanzo hadi Ufunuo... iko hivi: ukisoma kwa UMAKINI utagundua kuwa vitabu vya Mwanzo mpaka Malaki ni MAELEZO YA AHADI YA MUNGU (yameelezeaje?) Na Mathayo mpaka Yohana MTIMIZA AHADI AKIWA KATIKA MWILI PAMOJA NA USHAHIDI WA KUTIMIA KWA AHADI (eye witness account).

Matendo wa Mitume ni WANAFUNZI WAKIFUNDISHA HABARI YA AHADI KUTIMIA.

Warumi mpaka Ufunuo NI MAELEKEZO JUU YA WAAMINI WALIOPOKEA HIYO AHADI KATIKA NAMNA YA KUENENDA.

Maana ya Agano Jipya na Agano la Kale siyo uzee na upya wa maagano.

Kuhusu Maagano nitaelezea huko mbele.

Tuanze kwa kuangalia ***Waebrania 1:1-4***

***[1] Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,***

***[2] mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.***

***[3] Yeye kwa kuwa ni m_n_g_'a_o_ _wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya***

***uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu;***

***[4] amefanyika bora kupita malaika, kwa kadiri jina aliloliirithi lilivyo tukufu kuliko lao.***

Hii ni sawa na kusema Mungu (Ahadi yake) imezungumziwa kwa sehemu nyingi (hii sehemu siyo mahali bali Nyakati mbalimbali kwenye maandiko ndiyo maana KJV inatumia SUNDRY TIMES) na kwa namna nyingi (Hii ni lugha mbalimbali za maandiko matakatifu yaani Mwanzo hadi Malaki au mifano mbalimbali, vitu, watu, matukio n.k) kupitia manabii yaani Musa na wengine MWISHO wa Nyakati yaani au tuseme hakuna wakati mwingine ambapo Mungu atajifunua zaidi ya alivyojifunua katika Kristo Yesu ndiyo maana AMPLIFIED Bible wanatumia FINALITY.. Mwisho huu ni kujifunua katika Mwanae Yesu Kristo ambaye Yeye ni mnga'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake... yaani YEYE NDIYE ANAYEMDHIHIRISHA YA KUWA HIVI NDIVYO ALIVYO...

Ndiyo maana ukitaka kumjua Mungu ni lazima umtazame Yesu Kristo.

Ndiyo maana Yohana akaandika kwenye ***Yohana 1:18***

***[18] Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua.***

Yesu ndiye aliyemfunua Baba akawa wazi kwetu... hivyo mtu anayejifunza Mungu nje ya Yesu Kristo atakutana na vimeo vya kutosha na atayabandika majina kuwa ndiye Mungu wake.

Jesus is a SOLE expression of God's True Character; it's like saying if it's not in Jesus it's not in God.

Hakuna mtu atakayemtazama Yesu na bado awe na ujasiri wa kusema Mungu hachunguziki.

Hizo njia mbalimbali (Divers Manners) ambazo Mungu ametambulishwa kwenye maandiko ya Agano la Kale kupitia manabii, tunaweza kuanza kuziangalia leo.

Angalia wakati Yesu anahubiri Injili kwa Nicodemo alitumia matukio ya Musa na manabii kuelezea Ahadi ya Mungu ya Uzima wa milele.

Yesu alichukua vitu kadhaa na kufundisha uzima wa milele au Kuzaliwa upya au Kuzaliwa na Mungu au Kuzaliwa kwa maji au Kuzaliwa kwa Roho... sasa alitoa wapi?

Sasa NIKODEMO ni RABI au Mwalimu a.k.a Farisayo... Anayo elimu ya dini lakini hajui kuhusu

Kuzaliwa Upya... ndiyo maana usishangae mtu ana PhD ya THEOLOGY na asiwe na uzima wa milele ndani yake ili kajaza tu Mistari na hadithi kichwani...

Angalia ***Yohana 3:3-10***

***[3] Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.***

***[4] Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa?***

***[5] Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.***

***[6] Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho.***

***[7] Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili.***

***[8] Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho.***

***[9] Nikodemo akajibu, akamwambia, Yawezaje kuwa mambo haya?***

***[10] Yesu akajibu, akamwambia, Je! Wewe u mwalimu wa Israeli, na mambo haya huyafahamu?***

Haya maswala ya kuingia katika ufalme wa Mungu kwa Kuzaliwa Upya ndiyo Yesu kayatoa wapi? Kichwani? La Hasha...

***Yohana 3:5***

***[5] Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.***

Kwa maji na kwa Roho... ukisoma kwa haraka utafikiri ni vitu viwili tofauti ila ni kitu kimoja... Pale neno ***"NA"*** si kiunganishi tu kwa lugha ya Kigiriki bali INAELEZEA JAMBO... neno lililotumika ni ***kai*** na siyo ***de***

***De*** ni kiunganishi lakini ***kai*** ni kielezi cha jambo. Hivyo ni sawa na kusema KUZALIWA KWA ROHO ***AMBAKO*** NI KUZALIWA KWA MAJI.

Hii iko wapi? ***Ezekieli 36:25-28***

***[25] Nami nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi; nitawatakaseni na uchafu wenu wote, na vinyago vyenu vyote.***

***[26] Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe***

***uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama.***

***[27] Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda.***

***[28] Nanyi mtakaa katika nchi ile niliyowapa baba zenu, nanyi mtakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wenu.***

Angalia hayo Maneno. Maji kisha moyo, tena roho halafu watu wangu.

***Tito 3:4-7***

***[4] Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa;***

***[5] si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;***

***[6] ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu;***

***[7] ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu.***

Kutumia neno Kuoshwa na Kuzaliwa Upya huleta uhusiano na Yohana pamoja na Ezekieli.

Kisha akaendelea kumwambia Nikodemo ***Yohana 3:14-16***

***[14] Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa;***

***[15] ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye.***

***[16] Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.***

Kwa hiyo kitendo cha Musa kumwinua nyoka jangwani ni Injili ya Uzima wa milele. Kila aliyemtazama yule nyoka alipona hii ni sawa na kusema kila anayemwamini yule ALIYEINULIWA (KRISTO KWA MFANO WA NYOKA) HATAKUFA AU ATAKUWA NA UZIMA WA MILELE AU UZIMA WA MUNGU NDANI YAKE.

Kwa hiyo Ezekieli (nabii) na Musa WALIHUBIRI kitu kimoja kwa nyakati tofauti na kwa lugha Tofauti.

Mmoja alizungumzia KUNYUNYIZIWA MAJI, KUTAKASWA, KUPEWA MOYO MPYA, KUPEWA

ROHO WA MUNGU. NA KUFANYIWA WATU WA MUNGU.

Musa Yeye akamwinua Nyoka AMTAZAMAE AWE MZIMA...

TWO DIFFERENT PEOPLE, TWO DIFFERENT STYLES ONE MESSAGE. HALELUYA!!.

# SURA YA 12

## *KUNANI MATHAYO HADI UFUNUO?*

Kuna Baada ya kuona lengo la maandiko matakatifu (MWANZO mpaka MALAKI) ambazo ndiyo chanzo cha mambo yaliyoko kwenye vitabu vya MATHAYO hadi UFUNUO.

Hebu sasa twende kutazama zaidi hayo mambo yaliyoandikwa kutoka Musa, Manabii na Zaburi.

Angalia tena kwa ajili ya kujikumbusha.

***Yohana 5:39-40***

***[39] Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia.***

***[40] Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima.***

Yesu anaweka wazi kwamba Maandiko yamebeba ujumbe mmoja ambao ni YEYE.

Na Yesu ndiye anayeandikwa kule kwani ndani yako ndipo kuna uzima.

Kwenye Luka 24:25-27

***[25] Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii!***

***[26] Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?***

***[27] Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.***

Anasema Musa na Manabii aliandika habari zake… _ambapo ni kufa na kufufuka au kuingia katika utukufu wake.

Ujumbe huo anaurudia tena hapa mbele ya Thenashara...

***Luka 24:44-47***

***[44] Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.***

***[45] Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko.***

***[46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;***

***[47] na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.***

Au kwa ujumla vitabu 39 ni habari za Yesu Kristo, kufufuka ili watu wapate ondoleo la dhambi. Yohana anaandika ili watu wawe na uzima (**Yohana 5:40**) na huo uzima kwa sababu ni wa Mungu kwenye **Yohana 3:16** akauita ni wa milele.

Kwa hiyo Kuondolewa dhambi au Msamaha wa dhambi ni sawa kabisa na kusema KUPOKEA uzima wa milele au Uzima wa Mungu. Sawa na 1 Wakorintho 6:17

***1 Wakorintho 6:17***

***[17] Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye.***

Kwenye mtiririko huu utagundua Yesu alikuwa na Tabia ya kuita vitabu 39 yaani Mwanzo mpaka Malaki.

***1. Maandiko***

***2. Maandiko matakatifu***

***3. Unabii au manabii,***

***4. Musa na manabii,***

***5. Torati ya Musa, manabii na Zaburi.***

Hii namna mbalimbali ya kusema maandiko ya Agano la Kale (kama yalivyogawanywa kwenye Biblia zetu).

Yesu alianza kutoka Musa kwa sababu Musa ni mtu wa kwanza kuandika na wengine waliofuata walikuwa wakimnukuu.

Musa ndiye MWANDISHI pekee ambayo hakunukuu popote.

Musa hakuishi ENZI za Adamu, Habili, Henoko, Nuhu, Abrahamu, Isaka, Yakobo... ila alipata na kuandika haya yote kwa njia ya Kuhadithiwa (ORAL TRADITION) yeye akaweka katika Maandishi.

Hii inaonekana pia kwenye

***Zaburi** 78:1-7*

***[1] Enyi watu wangu, sikilizeni sheria yangu, Tegeni masikio kwa maneno ya kinywa changu.***

***[2] Na nifunue kinywa changu kwa mithali, Niyatamke mafumbo ya kale.***

***[3] Mambo tuliyoyasikia na kuyafahamu, Ambayo baba zetu walituambia.***

***[4] Hayo hatutawaficha wana wao, Huku tukiwaambia kizazi kingine, Sifa za BWANA, na nguvu zake, Na mambo yake ya ajabu aliyoyafanya.***

***[5] Maana alikaza ushuhuda katika Yakobo, Na sheria aliiweka katika Israeli. Aliyowaamuru baba zetu Wawajulishe wana wao,***

***[6] Ili kizazi kingine wawe na habari, Ndio hao wana watakaozaliwa. Wasimame na kuwaambia wana wao***

***[7] Wamwekee Mungu tumaini lao. Wala wasiyasahau matendo ya Mungu, Bali wazishike amri zake.***

Gideoni anasema kitu kile kile...

***Waamuzi 6:13***

***[13] Gideoni akamwambia, Ee Bwana wangu, ikiwa BWANA yu pamoja nasi, mbona mambo haya yote yametupata? Yako wapi matendo yake ya ajabu, WALIYOTUHADITHIA baba zetu, wakisema, Je! Siye***

***BWANA, aliyetuleta huku kutoka Misri? Ila sasa ametutupa, naye ametutia katika mikono ya Midiani.***

Kwa hiyo Musa ameandika habari za Yesu sawa sawa na Yohana 5:39,40 na Wayahudi tangu wakati wa Musa hawakuamini hilo na hata hao ambayo Yesu alikuwa anazungumza nayo pia hawakumwamini.

Musa alifanya nini kwa watu WASIOAMINI? ALIWASHTAKI.

***Yohana 5:45-47***

***[45] Msidhani kwamba mimi nitawashitaki kwa Baba; yuko anayewashitaki, ndiye Musa, mnayemtumaini ninyi.***

***[46] Kwa maana kama mngalimwamini Musa, mngeniamini mimi; kwa sababu yeye aliandika habari zangu.***

***[47] Lakini msipoyaamini maandiko yake, mtayaamini wapi maneno yangu?***

Kukataa kuamini ujumbe wa Musa ni kukataa kumwamini Yesu Kristo na kukataa kumwamini Kristo ni kukosa uzima wa milele.

Kwa hiyo wakiwa jangwani walimsumbua Musa kwa kutokuamini kwako. Ndiyo MWANDISHI wa Zaburi na

Waebrania anaitwa WALIFANYA MIOYO YAO KUWA MIGUMU.

***Zaburi 95:8-10***

***[8] Msifanye migumu mioyo yenu; Kama vile huko Meriba Kama siku ya Masa jangwani.***

***[9] Hapo waliponijaribu baba zenu, Wakanipima, wakayaona matendo yangu.***

***[10] Miaka arobaini nalihuzunika na kizazi kile, Nikasema, Hao ni watu waliopotoka mioyo, Hawakuzijua njia zangu.***

***Waebrania 3:7-12***

***[7] Kwa hiyo, kama anenavyo Roho Mtakatifu, Leo, kama mtaisikia sauti yake,***

***[8] Msifanye migumu mioyo yenu, Kama wakati wa kukasirisha, Siku ya kujaribiwa katika jangwa,***

***[9] Hapo baba zenu waliponijaribu, wakanipima, Wakaona matendo yangu miaka arobaini.***

***[10] Kwa hiyo nalichukizwa na kizazi hiki, Nikasema, Sikuzote ni watu waliopotoka mioyo hawa; Hawakuzijua njia zangu;***

***[11] Kama nilivyoapa kwa hasira yangu, Hawataingia rahani mwangu.***

***[12] Angalieni, ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai.***

Angalia

Mioyo migumu

Waliopotoka mioyo

Hawakujua njia za Mungu

Walikuwa na moyo mbovu wa KUTOKUAMINI.

KWA HUO MOYO MGUMU NI KUTOAMINI.

Kwenye hadhira ya Musa kulikuwa na watu WANAOMINI NA WASIOAMINI.

Angalia jinsi Yesu alivyojibu swali aliloulizwa kwa habari ya Musa.

***Marko 10:1-6***

***[1] A_k_a_o_n_d_o_k_a_ _h_u_k_o_ _a_k_a_f_i_k_a_ _m_i_p_a_k_a_n_i_ _m_w_a_ _U_y_a_h_u_d_i_,_ _n_a_ _n_g_'a_m_b_o_ _y_a_ _Y_o_r_d_a_n_i_;_ _makutano mengi wakakutanika tena wakamwendea; akawafundisha tena kama alivyozoea.***

***[2] Basi Mafarisayo wakamwendea, wakamwuliza, Je! Ni halali mtu kumwacha mkewe? Huku wakimjaribu.***

***[3] Naye akajibu, akawaambia, Musa aliwaamuru nini?***

***[4] Wakasema, Musa alitoa ruhusa kuandika hati ya talaka na kumwacha.***

***[5] Yesu akawaambia, Kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu aliwaandikia amri hii.***

***[6] Lakini tangu mwanzo wa kuumbwa ulimwengu, aliwafanya mume na mke.***

Hapa unaona Yesu alikuwa akifundisha… _bila shaka alikuwa anatumia vitabu vya Musa, manabii na Zaburi na kutoka kwenye vitabu hivyo wakauliza swali.

Sehemu walipotolea swali ni **Kumbukumbu 24:1-4**

Sehemu alipojibia Yesu ni **Mwanzo 2:24.**

Hivi vyote ni vitabu vya Musa Kuonyesha kwamba Musa aliwapa sheria Wayahudi kwa sababu ya kutokuamini.

Kama Musa aliandika mpango wa Mungu kwenye **Mwanzo 2:24** na kwa kuonyesha ya kuwa hawakuamini mpango huo wa Mungu, Musa aliwapa Amri au sheria kuonyesha ya kuwa hawaamini.

Ndiyo maana sheria siyo Mwamini bali kwa asiye amini.

Angalia ***1 Timotheo 1:6-11***

***[6] Wengine wakiyakosa hayo wamegeukia maneno ya ubatili;***

***[7] wapenda kuwa waalimu wa sheria, ingawa hawayafahamu wasemayo wala mambo yale wayanenayo kwa uthabiti.***

***[8] Lakini twajua ya kuwa sheria ni njema, kama mtu akiitumia kwa njia iliyo halali;***

***[9] AKILIFAHAMU NENO hili, ya kuwa sheria HAIMHUSU MTU WA HAKI, bali waasi, na wasio wataratibu, na makafiri, na wenye dhambi, na wanajisi, na wasiomcha Mungu, na wapigao baba zao, na wapigao mama zao, na wauaji,***

***[10] na wazinifu, na wafiraji, na waibao watu, na waongo, nao waapao kwa uongo; na likiwapo neno lo lote linginelo lisilopatana na mafundisho yenye uzima;***

***[11] kama vile ilivyonenwa katika Habari Njema ya utukufu wa Mungu ahimidiwaye, niliyowekewa amana.***

Kwa hiyo MUSA ALIANDIKA MAMBO YAHUSUYO: -

1. IMANI

2. KUTOKUAMINI

Kwa hiyo tumalize kwa kusema Musa alikuwa anaandika maombi yanayohusu imani na KUTOAMINI.

# SURA YA 13

## *AKAANZA KUTOKA MUSA*

Kuna Baada ya kuona ya kuwa Musa aliandika kuhusu Imani na KUTOAMINI kwenye vitabu vyake… _ni vyema ufahamu ya kuwa vitabu vya Musa vimeandikwa kwa mtiririko. Hii ina maana kitabu cha kwanza (Mwanzo) kina uhusiano na kitabu cha Pili (Kutoka), kitabu cha Pili, kina uhusiano na kitabu cha Tatu (Mambo ya Walawi), na kitabu cha tatu kina uhusiano na kitabu cha nne (Hesabu) na kitabu cha tano (Kumbukumbu la Torati).

Kwa mfano.

Umesoma Kutoka umekutana na SABATO,

***Kutoka 20:8-11***

***[8] Ikumbuke siku ya Sabato uitakase.***

***[9] Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote;***

***[10] lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako.***

***[11] Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.***

ILI UELEWE KUHUSU SABATO HUWEZI KUANZIA HAPA. LAZIMA UTAJIKWAA INABIDI URUDI KWENYE KITABU CHA MWANZO… _

***Mwanzo 2:1-3***

***[1] Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote.***

***[2] Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya.***

***[3] Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya.***

Umeona uhusiano?

Fikiria umeanzia...

***Kumbukumbu la Torati 5:1-3***

***[1] Musa akawaita Israeli wote, akawaambia, Enyi Israeli, zisikieni amri na hukumu ninenazo masikioni mwenu leo, mpate kujifunza na kuangalia kuzitenda.***

***[2] BWANA, Mungu wetu, alifanya agano nasi katika Horebu.***

***[3] BWANA hakufanya agano hili na baba zetu, bali na sisi, yaani, sisi sote tuliopo hapa, tu hai.***

Swali la kwanza ni kutaka Kurudi nyuma...

HUKO HOREBU WALIPEWA AGANO GANI?

Hii utaiona kwa undani ukirudi Kutoka 33 kuanzia mstari wa 6.

Hii haishii tu kwa vitabu vya Musa, utaona hata Yoshua, Waamuzi, Samweli, Wafalme, Zaburi hadi Malaki wametumia vitabu vya Musa.

Angalia ***1 Samweli 12:6***

***[6] Samweli akawaambia watu, Ni yeye BWANA aliyewaweka Musa na Haruni, ndiye yeye aliyewatoa baba zenu kutoka nchi ya Misri.***

AME REFER KITABU CHA MUSA "KUTOKA"

Kwa hiyo kitabu cha Mwanzo ni BASE YA VITABU VYOTE. UKISHAVURUGWA MWANZO, UTAFUNIKWA TU NA UFUNUO WA YOHANA.

Kitabu cha Mwanzo ni kitabu pekee ambacho hakikunukuu chochote popote...

Vitabu vingine vilivyofuata vitabu vya Musa vimenukuu kwenye maandiko ya Musa.

Angalia ***1 Wafalme 8:56***

***[56] Na ahimidiwe BWANA, aliyewapa watu wake Israeli kustarehe, vile vile kama yote aliyoyaahidi. Halikukosa kupatikana neno lo lote katika ahadi yake njema, aliyoahidi kwa mkono wa Musa, mtumishi wake.***

Wamerudi kwa Musa pia… _

***2 Wafalme 18:6***

***[6] Maana alishikamana na BWANA, hakuacha kumfuata, bali alizishika amri zake BWANA alizomwamuru Musa.***

***1 Mambo ya Nyakati 15:15***

***[15] Na wana wa Walawi wakalichukua sanduku la Mungu mabegani mwao kwa miti yake, kama vile Musa alivyoamuru, sawasawa na neno la BWANA.***

***2 Mambo ya Nyakati 30:16***

***[16] Wakasimama mahali pao kwa taratibu yao, sawasawa na torati ya Musa, mtu wa Mungu; nao makuhani wakainyunyiza damu, waliyoipokea mikononi mwa Walawi.***

***Ezra 6:18-19***

***[18] Wakawaweka makuhani katika kura zao, wakawaweka na Walawi katika zamu zao, kwa ajili ya huduma ya Mungu, iliyokuwako Yerusalemu; vile vile kama vilivyoandikwa katika chuo cha Musa.***

***[19] Kisha, wana wa uhamisho wakaifanya Pasaka, mwezi wa kwanza siku ya kumi na nne ya mwezi.***

***Nehemia 9:13-14***

***[13] Tena ulishuka juu ya mlima Sinai, ukasema nao toka mbinguni, ukawapa hukumu za haki, na sheria za kweli, na amri nzuri na maagizo;***

***[14] ukawajulisha sabato yako takatifu, na kuwaagiza maagizo, na amri, na sheria, kwa mkono wa mtumishi wako, Musa.***

***Zaburi 77:20***

***[20] Uliwaongoza watu wako kama kundi, Kwa mkono wa Musa na Haruni.***

***Zaburi 106:7***

***[7] Baba zetu katika Misri Hawakufikiri matendo yako ya ajabu; Hawakukumbuka wingi wa fadhili zako; Wakaasi penye bahari, bahari ya Shamu.***

***Isaya 63:11-14***

***[11] Ndipo alipozikumbuka siku za kale, za Musa, na watu wake, akisema, Yuko wapi yeye aliyewapandisha toka baharini pamoja na wachungaji wa kundi lake? Yuko wapi yeye aliyetia kati yao Roho yake Mtakatifu?***

***[12] Aliyewaongoza kwa mkono wake mtukufu, kwa mkono wa kuume wa Musa? Aliyeyatenga maji mbele yao, ili ajifanyie jina la milele?***

***[13] Aliyewaongoza vilindini, kama farasi jangwani, wasijikwae?***

***[14] K_a_m_a_ _n_g_'o_m_b_e_ _w_a_s_h_u_k_a_o_ _b_o_n_deni, Roho ya BWANA akawastarehesha; ndivyo ulivyowaongoza watu wako, ili ujifanyie jina lenye utukufu.***

***Yeremia 2:6***

***[6] Wala hawakusema, Yuko wapi BWANA, aliyetutoa katika nchi ya Misri; akatuongoza jangwani, katika nchi ya ukame na mashimo, katika nchi ya kiu na ya kivuli cha mauti, katika nchi ambayo ndani yake hapiti mtu, wala haikukaliwa na watu?***

***Ezekieli 20:9***

***[9] Lakini nalitenda kwa ajili ya jina langu, ili lisitiwe unajisi mbele ya macho ya mataifa, ambao walikaa pamoja nao, ambao machoni pao nalijidhihirisha kwao, kwa kuwatoa katika nchi ya Misri.***

***Danieli 9:11***

***[11] Naam, Israeli wote wameihalifu sheria yako, kwa kugeuka upande, wasiisikilize sauti yako; basi kwa hiyo laana imemwagwa juu yetu, na uapo ule ulioandikwa katika sheria ya Musa, mtumishi wa Mungu; kwa sababu tumemtenda dhambi.***

***Hosea 8:1***

***[1] Tia baragumu kinywani mwako. Kama tai, anakuja juu ya nyumba ya BWANA; kwa sababu wamelihalifu agano langu, wameiasi sheria yangu.***

***Yoeli 1:9***

***[9] Sadaka ya unga na sadaka ya kinywaji Zimekatiliwa mbali na nyumba ya BWANA; Hao makuhani, wahudumu wa BWANA, wanaomboleza.***

***Amosi 3:1***

***[1] Lisikieni neno hili alilolisema BWANA juu yenu, enyi wana wa Israeli, juu ya jamaa yote niliowapandisha kutoka nchi ya Misri, nikisema,***

***Obadia 1:18***

***[18] Na nyumba ya Yakobo itakuwa moto, na nyumba ya Yusufu itakuwa mwali wa moto, na nyumba ya Esau itakuwa mabua makavu, nao watawaka kati yao, na kuwateketeza; wala hatasalia mtu awaye yote katika nyumba ya Esau; kwa kuwa BWANA amesema hayo.***

Sasa unaweza kupata muda wa kuangalia kitabu kimoja baada ya kingine, utagundua hakuna jambo walitengeneza hewani ila kwa kutumia vitabu vya Musa.

Vitabu vya Musa ni vitabu muhimu sana kwenye IMANI YETU, NI MSINGI HASA.

# SURA YA 14

## *MATHAYO, MARKO, LUKA NA YOHANA*

KUna Baada ya kuangalia uhusiano wa vitabu vya Musa na vitabu vilivyofuata (manabii na Zaburi) sasa tuangalie Vitabu Vinne vya Injili. Yaani Mathayo, Marko, Luka na Yohana.

Tumeshaweka msingi ya kuwa vitabu vya Agano la Kale (Mwanzo mpaka Malaki) ni vitabu vya Ahadi ya ukombozi au unabii juu ya Ahadi hiyo. Na tukaweka msingi kuwa kitabu cha Mwanzo ni kitabu mama kwenye vitabu vya Agano la Kale kwani ndiyo Mwanzo wa kila kitu, wala chenyewe hakijanukuu kitabu kingine kile.

Vitabu vinne vya Musa vitaeleweka tu kama mtu ameshasoma kwa mtiririko kuanzia kitabu cha Mwanzo.

Jambo lingine tulililoliona ni kwamba; baada ya vitabu vya Musa... vitabu vyote vilivyofuata vinatoa habari zake kutoka kwenye vitabu vitano vya Musa yaani manabii na Zaburi. (Yoshua mpaka Malaki).

MANABII WOTE WA AGANO LA KALE NI WANAFUNZI WA MUSA KWA LUGHA RAHISI KABISA....

Vipi kuhusu vitabu vya Injili?

Mathayo, Marko, Luka na Yohana?

Hivi vinaitwa VITABU VYA USHAHIDI WA MACHO. USHAHIDI wa nini? Yale ambayo Musa na Manabii walitabiri kwa nguvu. Waandishi wa vitabu hivyo waliandika utimilifu wa yale yaliyoandikwa kama AHADI KWENYE MAANDIKO YA MUSA, MANABII NA ZABURI.

Luka anaanza kitabu chake kwa kuonyesha kuwa ni barua yenye utafiti wake juu ya YALE YALIYOTIMIZWA...

***Luka 1:1-4***

***[1] Kwa kuwa watu wengi wametia mikono kutunga kwa taratibu habari za MAMBO YALE YALIYOTIMIZWA KATIKATI YETU,***

***[2] kama walivyotuhadithia wale waliokuwa mashahidi wenye kuyaona, na watumishi wa lile neno tokea mwanzo,***

***[3] nimeona vema mimi nami, kwa kuwa nimejitafutia usahihi wa mambo hayo yote tangu mwanzo, kukuandikia kwa taratibu, Theofilo mtukufu,***

***[4] upate kujua hakika ya mambo yale uliyofundishwa.***

Na kwenye SUMMARY yake mwishoni anazungumza kuwa mambo aliyoyasema Yesu Kristo huko ndani ni habari za kufa na kufufuka kwake ambao siyo ujumbe

uliochukuliwa hewani bali ni wa Musa, manabii na Zaburi… _

Angalia... ***Luka 24:44-46***

***[44] KISHA AKAWAAMBIA, HAYO NDIYO MANENO YANGU NILIYOWAAMBIA nilipokuwa nikali PAMOJA NANYI, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika TORATI YA MUSA, na katika MANABII na ZABURI.***

***[45] Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko.***

***[46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba KRISTO ATATESWA NA KUFUFUKA SIKU YA TATU;***

Luka pia ameonyesha ukoo wa Yesu... hadi Adamu, hivyo ameenda mpaka kitabu cha Mwanzo.

***Luka 3:23,36-38***

***[23] Na Yesu mwenyewe, alipoanza kufundisha, alikuwa amepata umri wake kama miaka thelathini, akidhaniwa kuwa ni mwana wa Yusufu, wa Eli,***

***[36] wa Kenani, wa Arfaksadi, wa Shemu, wa Nuhu, wa Lameki,***

***[37] wa Methusela, wa Henoko, wa Yaredi, wa Mahalaleli, wa Kenani,***

***[38] wa Enoshi, wa Sethi, wa Adamu, wa Mungu.***

Namna ya Mathayo ilikuwa tofauti kidogo, anaanza kwa kuwatambulisha watu wawili muhimu sana kwenye historia ya Wayahudi... IBRAHIM NA DAUDI.

Hapo ni kitabu cha Mwanzo (Musa) na kitabu cha Nabii (Samweli).

***Mathayo 1:1,17***

***[1] Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahimu.***

***[17] Basi vizazi vyote tangu Ibrahimu hata Daudi ni vizazi kumi na vinne; na tangu Daudi hata ule uhamisho wa Babeli ni vizazi kumi na vinne; na tangu ule uhamisho wa Babeli hata Kristo ni vizazi kumi na vinne.***

Kutaja msururu wa majina ya watu tangu Ibrahimu mpaka Yesu ni hakika ya kuwa amepitia vitabu vingi vya Agano la Kale.

Mathayo hakuandika tu kwa lengo la kuandika bali alitaka kumwonyesha Kristo na alipoanzia KWA IBRAHIMU.

Namna ya Marko ilikuwa tofauti pia, lakini alianza Agano la Kale kwenye unabii wa Isaya. Unaomtambulisha Yohana ambaye na yeye alimtambulisha Yesu Kristo.

Angalia ***Marko 1:1-2***

***[1] Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.***

***[2] Kama ilivyoandikwa katika nabii Isaya, Tazama, namtuma mjumbe wangu***

***Mbele ya uso wako, Atakayeitengeneza njia yako.***

Yohana anaanza namna yake ya tofauti kabisa kwa kuchambua Mwanzo 1.

Angalia ***Yohana 1:1-5***

***[1] Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.***

***[2] Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.***

***[3] Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika.***

***[4] Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu.***

***[5] N_a_y_o_ _n_u_r_u_ _y_a_n_g_'a_a_ _g_i_z_a_n_i_,_ _w_a_l_a_ _g_i_z_a_ _h_a_l_i_k_u_i_w_e_z_a_._ _***

Angalia ... ***Mwanzo 1:1-3***

***[1] Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi.***

***[2] Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji.***

***[3] Mungu akasema, Iwe nuru; ikawa nuru.***

Katika mazingira haya yote unagundua kuwa Vitabu Vinne vya Injili havijajiegesha bali ni USHAHIDI wa Macho kwa yale yaliyotabiriwa kwenye maandiko ya Agano la Kale.

NI HATARI KUHISI YA KWAMBA VITABU VYA AGANO JIPYA VINAJITEGEMEA.

ILA NI HEKIMA KUJUA YA KWAMBA VITABU VYA AGANO JIPYA VINATEGEMEA VITABU VYA AGANO LA KALE.

# SURA YA 15

## *MATHAYO NA AGANO LA KALE*

Kuna waandishi vitabu Vinne  hawakuandika tu habari za Yesu ili mradi bali waliweka msisitizo wa yale yaliyokwisha andikwa na Musa na manabii sasa twende kwenye kitabu kimoja baada ya kingine.

Inawezekana kuna mambo mengi ambayo Yesu alifanya, mfano kupika, kuranda mbao na Baba yake Yusufu, kuteka maji, au kucheza mpira, n.k. lakini waandishi wa

Injili wameyachagua kimaalumu kabisa matukio yanayohusu huduma yake na ukombozi wa mwanadamu.

Sasa haya wameyafanya kwa UMAKINI mkubwa tena kwa kuhusisha kwa kiasi kikubwa maandiko ya Agano la Kale.

Kwa USHAHIDI zaidi tuangalie....

Mwanzo kabisa Mathayo anaonyesha Kuzaliwa kwa Yesu ni jambo lililotabiriwa na manabii.

***Mathayo 1:20-23***

***[20] Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu.***

***[21] Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.***

***[22] Hayo yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema,***

***[23] Tazama, bikira atachukua mimba, Naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake Imanueli; Yaani, Mungu pamoja nasi.***

Mathayo ALITOA hili katika ***Isaya 7:14***

***[14] Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli.***

Kwenye Mathayo 2:3-6

***[3] Basi mfalme Herode aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye.***

***[4] Akakusanya wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu, akatafuta habari kwao, Kristo azaliwa wapi?***

***[5] Nao wakamwambia, Katika Bethlehemu ya Uyahudi; kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na nabii,***

***[6] Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Yuda, Hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda; Kwa kuwa kwako atatoka mtawala Atakayewachunga watu wangu Israeli.***

Angalia KWA MAANA NDIVYO ILIVYOANDIKWA NA NABII (Agano la Kale) ...

KUANZIA HAPA SITANUKUU MISTARI YOTE YA AGANO LA KALE ILA UNAWEZA KUTUMIA "CROSS REFERENCE" chini au kulia kwa Biblia yako kuona mahali nabii aliponukuu… _SAWA?

***Mathayo 2:16-18***

***[16] Ndipo Herode, alipoona ya kuwa amedhihakiwa na wale mamajusi, alighadhabika sana, akatuma watu akawaua watoto wote wanaume waliokuwako huko Bethlehemu na viungani mwake mwote, tangu wenye miaka miwili na waliopungua, kwa muda ule aliouhakikisha kwa wale mamajusi.***

***[17] Ndipo lilipotimia neno lililonenwa na nabii Yeremia, akisema,***

***[18] Sauti ilisikiwa Rama, Kilio, na maombolezo mengi, Raheli akiwalilia watoto wake, Asikubali kufarijiwa, kwa kuwa hawako.***

Hapa amemnukuu YEREMIA....

Huduma ya MTANGULIZI wake Yohana Mbatizaji na yenyewe haikutoka hewani...

Angalia ***Mathayo 3:1-3***

***[1] Siku zile aliondokea Yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema,***

***[2] Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.***

***[3] Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema, Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake.***

NABII ISAYA ALITABIRI.

***Mathayo 12:15-21***

***[15] Naye Yesu hali akiyafahamu hayo akaondoka huko; na watu wengi wakamfuata; akawaponya wote,***

***[16] akawakataza wasimdhihirishe;***

***[17] ili litimie neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema,***

***[18] Tazama, mtumishi wangu niliyemteua; Mpendwa wangu, moyo wangu uliyependezwa naye; Nitatia roho yangu juu yake, Naye atawatangazia Mataifa hukumu.***

***[19] Hatateta wala hatapaza sauti yake; Wala mtu hatasikia sauti yake njiani.***

***[20] Mwanzi uliopondeka hatauvunja, Wala utambi utokao moshi hatauzima,***

***Hata ailetapo hukumu ikashinda.***

***[21] Na jina lake Mataifa watalitumainia.***

ISAYA TENA....

***Mathayo 12:38-41***

***[38] Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.***

***[39] Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa ishara, ila ishara ya nabii Yona.***

***[40] Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.***

***[41] Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.***

Kawanukuu YONA, 1 WAFALME 10:1 NA 2 MAMBO YA NYAKATI 9:1

***Mathayo 13:13-16***

***[13] Kwa sababu hii nasema nao kwa mifano; kwa kuwa wakitazama hawaoni, na wakisikia hawasikii, wala kuelewa.***

***[14] Na neno la nabii Isaya linatimia kwao, likisema, Kusikia mtasikia, wala hamtaelewa; Kutazama mtatazama, wala hamtaona.***

***[15] Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, Na kwa masikio yao hawasikii vema, Na macho yao***

***wameyafumba; Wasije wakaona kwa macho yao, Wakasikia kwa masikio yao, Wakaelewa kwa mioyo yao, Wakaongoka, nikawaponya.***

***[16] Lakini, heri macho yenu, kwa kuwa yanaona; na masikio yenu, kwa kuwa yanasikia.***

NABII ISAYA TENA...

***Mathayo 21:1-5***

***[1] Hata walipokaribia Yerusalemu, na kufika Bethfage, katika mlima wa Mizeituni, ndipo Yesu alipotuma wanafunzi wawili akiwaambia,***

***[2] Enendeni mpaka kijiji kile kinachowakabili, na mara mtaona punda amefungwa, na mwana-punda pamoja naye; wafungueni mniletee.***

***[3] Na kama mtu akiwaambia neno, semeni, Bwana anawahitaji; na mara huyo atawapeleka.***

***[4] Haya yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema,***

***[5] Mwambieni binti Sayuni Tazama, mfalme wako anakuja kwako, Mpole, naye amepanda punda, Na mwana-punda, mtoto wa punda.***

ZEKARIA 9:9

***Mathayo 26:51-56***

***[51] Na tazama, mmoja wao waliokuwa pamoja na Yesu akanyosha mkono wake, akaufuta upanga wake, akampiga mtumwa wa Kuhani Mkuu, akamkata sikio.***

***[52] Ndipo Yesu akamwambia, Rudisha upanga wako mahali pake, maana wote waushikao upanga, wataangamia kwa upanga.***

***[53] Ama wadhani ya kuwa mimi siwezi kumsihi Baba yangu, naye ataniletea sasa hivi zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika?***

***[54] Yatatimizwaje basi maandiko, ya kwamba hivyo ndivyo vilivyopasa kujiri?***

***[55] Saa ile Yesu akawaambia makutano, Je, mmetoka kama kumkamata m_n_y_a_n_g_'a_n_y_i_,_ _w_e_n_y_e_ _p_a_n_g_a_ _n_a_ _m_a_r_u_n_g_u_,_ _ili kunishika? Kila siku naliketi hekaluni nikifundisha, msinikamate.***

***[56] Lakini haya yote yamekuwa, ili maandiko ya manabii yatimizwe. Ndipo wanafunzi wote wakamwacha, wakakimbia.***

Hapa ametaja JUMLA...

MAANDIKO YA MANABII YATIMIZWE.

HII NI AGANO LA KALE KWA UJUMLA WAKE.

Hata jinsi alivyojibu maswali yake na kushinda MAJARIBU alifafanua maandiko ya Agano la Kale.

***Mathayo 12:1-8***

***[1] Wakati ule Yesu alipita katika mashamba siku ya sabato; wanafunzi wake wakaona njaa, wakaanza kuvunja masuke, wakala.***

***[2] Na Mafarisayo walipoona, walimwambia, Tazama! Wanafunzi wako wanafanya neno ambalo si halali kulifanya siku ya sabato.***

***[3] Akawaambia, Hamkusoma alivyotenda Daudi, alipokuwa na njaa, yeye na wenziwe?***

***[4] jinsi alivyoingia katika nyumba ya Mungu, akaila mikate ile ya wonyesho, ambayo si halali kwake kuila wala kwa wale wenziwe, ila kwa makuhani peke yao?***

***[5] Wala hamkusoma katika torati, kwamba siku ya sabato makuhani hekaluni huinajisi sabato wasipate hatia?***

***[6] Lakini nawaambieni, kwamba hapa yupo aliye mkuu kuliko hekalu.***

***[7] Lakini kama mngalijua maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka, msingaliwalaumu wasio na hatia.***

***[8] Kwa maana Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato.***

HAPA WALIMUULIZA SWALI LA **Kutoka 20:9-11** akajibu kwa kutumia Mambo ya Walawi 24:9, 1 Samweli 21:1-6, Hesabu 28:9,10, na Hosea 6:6.

***Mathayo 19:3-6***

***[3] Basi Mafarisayo wakamwendea, wakamjaribu, wakimwambia, Je! Ni halali mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu?***

***[4] Akajibu, akawaambia, Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke,***

***[5] akasema, Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja?***

***[6] Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe.***

Hapo alijibu kwa kutumia kitabu cha Musa yaani **Mwanzo 2:24**

Wakaendelea kuuliza ***Mathayo 19:7-8***

***[7] Wakamwambia, Jinsi gani basi Musa aliamuru kumpa hati ya talaka, na kumwacha?***

***[8] Akawaambia, Musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu; lakini tangu mwanzo haikuwa hivi.***

WALIULIZA KUTOKEA KUMBUKUMBU LA TORATI 24:1-4 AKAWAJIBU KUTUMIA TENA kitabu cha MWANZO...

Sasa tungeweza kuendelea zaidi na zaidi,

Utaona SEHEMU nyingi Mathayo alionyesha kuwa kitabu cha Injili ya Mathayo haijaelea hewani bali inategemea Mwanzo mpaka Malaki.

Ndiyo maana utaona.

HAMKUSOMA,

IMEANDIKWA,

KAMA ILIVYOANDIKWA,

IMENENWA,

ILI LITIMIE,

MAANDIKO MATAKATIFU

N.K.

Hii itakufanya uone kuwa Biblia ni kitabu kinachohusiana Mwanzo mpaka Ufunuo.

(Unaweza pia kuchambua Marko, Luka na Yohana na kuona jinsi ambavyo vitabu hivyo vinaasisiwa na Maandiko Matakatifu yaani Mwanzo mpaka Malaki).

# SURA YA 16

## *MATENDO YA MITUME NA AGANO LA KALE*

Tumemtumia Mathayo kama mwakilishi wa vitabu vingine vya injili, kwa hiyo tunaweza kuachana na Marko, Luka na Yohana kwa sasa na kuelekea Matendo ya Mitume. Hamasa ya waandishi wa Mathayo hadi Yohana ni ahadi ya Mungu ya ukombozi kwenye Maandiko ya Agano la Kale. Sasa leo tuangalie MATENDO YA MITUME.

Kuna ujumbe gani hasa kwenye Kitabu cha pili cha Luka kiitwacho Matendo ya Mitume?

Luka anaanza kwa kusema ... ***Matendo ya Mitume 1:1***

***[1] Kitabu kile cha kwanza nalikiandika, Theofilo, katika habari ya mambo yote aliyoanza Yesu kufanya na kufundisha,***

(Bila shaka UNAKUMBUKA kwamba kitabu cha kwanza cha Luka ni Injili ya Luka na zote ziliandikwa kwa mtu mmoja - Theofilo) angalia

Luka 1:1-4

***[1] Kwa kuwa watu wengi wametia mikono kutunga kwa taratibu habari za mambo yale yaliyotimizwa katikati yetu,***

***[2] kama walivyotuhadithia wale waliokuwa mashahidi wenye kuyaona, na watumishi wa lile neno tokea mwanzo,***

***[3] nimeona vema mimi nami, kwa kuwa nimejitafutia usahihi wa mambo hayo yote tangu mwanzo, kukuandikia kwa taratibu, Theofilo mtukufu,***

***[4] upate kujua hakika ya mambo yale uliyofundishwa.***

Sasa kitabu cha Matendo ya Mitume generally imebeba ushuhuda wa mitume juu ya mateso ya Yesu, kufa na kufufuka kwake, na matokeo ya kazi hiyo ambayo ni WOKOVU au suluhisho la dhambi kupatikana.

Tunategemea kuona mitume wakitii agizo la Yesu la kuhubiri hayo hayo na siyo mengine kabisa.

Yesu aliagiza... ***Marko 16:15-18***

***[15] Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.***

***[16] Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.***

***[17] Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;***

***[18] watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya***.

MKAHUBIRI MAANA YAKE MKATANGAZE (Kutangaza siyo kutengeneza jambo, ni kusema ulichopewa... unakuwa mjumbe tu).

MTANGAZAJI HUWA ANAFUATA SCRIPT YA WENYE TUKIO AU JAMBO LINALOTAKIWA KUTANGAZWA… _Hawezi kusema "nimepewa tangazo la mafuta ya alizeti, wameandika wasipewe watoto aaah ila mimi naongeza wasipewe na akina mama wajawazito" huwezi kufanya kitu kama hicho.

Ukiangalia pale maneno "kila KIUMBE" unaweza kuanza kuhubiria ng'ombe, chumvi, mashamba, n.k.

lakini Mathayo anaweza KUFUTA huo mtazamo... kwamba kila KIUMBE pale ni watu... angalia

***Mathayo 28:19-20***

***[19] Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;***

***[20] na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.***

Kwa hiyo KILA KIUMBE wa Marko ndiyo Mataifa wa Mathayo.

Luka anaandika ***Luka 24:44,46-48***

***[44] Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.***

***[46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;***

***[47] na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.***

***[48] Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya.***

KUHUBIRI INJILI KWA KILA KIUMBE = KUWAFANYA MATAIFA KUWA WANAFUNZI = KUWAFUNDISHA KUYASHIKA YOTE.

Luka anaweka hivi... na kwamba MATAIFA YOTE WATAHUBIRIWA KWA JINA LAKE HABARI YA TOBA NA ONDOLEO LA DHAMBI wakianzia Yerusalemu.

**Je, hii walitii na kufanya... tuangalie walifanyeje?**

SIKU YA PENTEKOSTE... Baada ya watu kukusanyika kwa mara ya kwanza Paulo anasimama kuhubiri… _

***Matendo ya Mitume 2:14-21***

***[14] Lakini Petro akasimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapaza sauti yake, akawaambia, Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu.***

***[15] Sivyo mnavyodhani; watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana;***

***[16] lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli,***

***[17] Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto.***

***[18] Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake Roho yangu, nao watatabiri.***

***[19] Nami nitatoa ajabu katika mbingu juu, na ishara katika nchi chini, damu na moto, na mvuke wa moshi.***

***[20] Jua litageuka kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla ya kuja ile siku ya Bwana iliyo kuu na iliyo dhahiri.***

***[21] Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa.***

Anaanza moja kwa moja kwa KUNUKUU na KUTAFSIRI YOELI

***Yoeli 2:28-32***

***[28] Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono;***

***[29] tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile, nitamimina roho yangu.***

***[30] Nami nitaonyesha mambo ya ajabu katika mbingu na katika dunia, damu, na moto, na minara ya moshi.***

***[31] Jua litageuzwa kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla haijaja hiyo siku ya BWANA iliyo kuu na itishayo.***

***[32] Na itakuwa ya kwamba mtu awaye yote atakayeliita jina la BWANA ataponywa; kwa kuwa katika mlima Sayuni na katika Yerusalemu watakuwako watu watakaookoka, kama BWANA alivyosema; na katika mabaki, hao awaitao BWANA.***

Hakuishia hapo tu... baada ya kuonyesha KUJAA ROHO NI KITU KILICHOTABIRIWA... ALIENDELEA...

***Matendo ya Mitume 2:22-24***

***[22] Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya: Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua;***

***[23] mtu huyu alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake tangu zamani, ninyi mkamsulibisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamwua;***

***[24] ambaye Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao.***

Hapa anaanza kuelezea MAUTI ya Yesu Kristo na KUFUFUKA KWAKE...

Lakini hakutaka iwe imekaa hewani alienda moja kwa moja kwenye Zaburi ya Daudi...

Angalia....

***Matendo ya Mitume 2:25-28***

***[25] Maana Daudi ataja habari zake, Nalimwona Bwana mbele yangu siku zote,***

***Kwa kuwa yuko upande wa mkono wangu wa kuume, nisitikisike.***

***[26] Kwa hiyo moyo wangu ukapendezewa, ulimi wangu ukafurahi; Tena mwili wangu nao utakaa katika matumaini.***

***[27] Kwa maana hutaiacha roho yangu katika kuzimu; Wala hutamtoa Mtakatifu wako aone uharibifu.***

***[28] Umenijuvisha njia za uzima; Utanijaza furaha kwa uso wako.***

Hii Zaburi iko Zaburi 16:8-11

***Zaburi 16:8-11***

***[8] Nimemweka BWANA mbele yangu daima, Kwa kuwa yuko kuumeni kwangu, sitaondoshwa.***

***[9] Kwa hiyo moyo wangu unafurahi, Nao utukufu wangu unashangilia, Naam, mwili wangu nao utakaa kwa kutumaini.***

***[10] Maana hutakuachia kuzimu nafsi yangu, Wala hutamtoa mtakatifu wako aone uharibifu.***

***[11] Utanijulisha njia ya uzima; Mbele za uso wako ziko furaha tele; Na katika mkono wako wa kuume Mna mema ya milele.***

Haya ni Maneno ya Daudi… _alisema kama anajisema MWENYEWE kumbe alisimama kama MFANO WA KRISTO (Ndiyo maana ni vyema kuwa makini unaposoma ZABURI).

Sasa Petro ALITAFSIRIJE hiyo Zaburi?

Angalia...

***Matendo ya Mitume 2:29-33***

***[29] Waume, ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo.***

***[30] Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi;***

***[31] yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu.***

***[32] Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake.***

***[33] Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia.***

DAUDI KAFA NA KABURI LAKE LIPO... LAKINI YESU AMEFUFUKA NA KABURI LIKO WAZI...

Hivyo Daudi alitabiri UFUFUO WA YESU KRISTO.

kwa hiyo kwenye matendo ya mitume Petro alihubiri alitumia Agano la Kale.

Baada ya Petro na Yohana kumwinua yule kiwete, nafasi ya kuhubiri ikawa wazi...

Angalia alipotolea mahubiri yake...

***Matendo ya Mitume 3:13-26***

***[13] Mungu wa Ibrahimu na wa Isaka na wa Yakobo, Mungu wa baba zetu, amemtukuza mtumishi wake***

***Yesu, ambaye ninyi mlimsaliti na kumkana mbele ya Pilato, alipokuwa ametoa hukumu yake afunguliwe.***

***[14] Bali ninyi mlimkana yule Mtakatifu, yule Mwenye haki, mkataka mpewe mwuaji;***

***[15] mkamwua yule Mkuu wa uzima, ambaye Mungu amemfufua katika wafu; na sisi tu mashahidi wake.***

***[16] Na kwa imani katika jina lake, jina lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemwona na kumjua; na imani ile iliyo kwake yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote.***

***[17] Basi sasa, ndugu, najua ya kuwa mliyatenda haya kwa kutokujua kwenu, kama na wakuu wenu walivyotenda.***

***[18] Lakini mambo yale aliyohubiri Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake wote, (MWANZO HADI MALAKI) ya kwamba Kristo wake atateswa, ameyatimiza hivyo.***

***[19] Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana;***

***[20] apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani;***

***[21] ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu.***

***[22] Kwa maana Musa kweli alisema ya kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi.***

***[23] Na itakuwa ya kwamba kila mtu asiyemsikiliza nabii huyo ataangamizwa na kutengwa na watu wake.***

***[24] Naam, na manabii wote tangu Samweli na wale waliokuja baada yake, wote walionena, walihubiri habari za siku hizi.***

***[25] Ninyi mmekuwa watoto wa manabii na wa maagano yale, ambayo Mungu aliagana na baba zenu, akimwambia Ibrahimu, Katika uzao wako kabila zote za ulimwengu zitabarikiwa.***

***[26] Mungu, akiisha kumfufua mtumishi wake Yesu, alimtuma kwenu ninyi kwanza, ili kuwabarikia kwa kumwepusha kila mmoja wenu na maovu yake.***

Mstari wa 18 anataja jumla ya vitabu vya Agano la Kale ALIYOHUBIRI TANGU MWANZO… _

Kisha anaendelea mbele kunukuu Maneno ya Musa… _akiyatoa KWENYE ***Kumbukumbu la Torati 18:15,18-19***

***[15] BWANA, Mungu wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye.***

***[18] Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru.***

***[19] Hata itakuwa, mtu asiyesikiliza maneno yangu atakayosema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake.***

Kwa hiyo huyo nabii aliyekuwa ANATAJWA na Musa ni KRISTO wala siyo Samweli.

Hivi ndivyo Petro alivyotafsiri maneno ya Musa.

Wewe unayachukuliaje maneno ya Musa? Unayatafsiri kwa jicho la ufunuo wa Kristo?

Kwenye sura ya nne baada ya kupigwa marufuku wasihubiri kwa jina la Yesu Kristo. Wakaenda kwa ndugu wengine wakaingia kwenye maombi.

Luka anarekodi baadhi ya mambo yaliyojadiliwa kabla ya kuanza kuomba na kujazwa Roho Mtakatifu.

Angalia hapa ***Matendo ya Mitume 4:24-28***

***[24] Nao waliposikia, wakampazia Mungu sauti zao kwa moyo mmoja, wakisema, Mola, wewe ndiwe Mungu, ndiwe uliyefanya mbingu na nchi na bahari na vitu vyote vilivyomo;***

***[25] nawe ulinena kwa Roho Mtakatifu kwa kinywa cha babaetu Daudi, mtumishi wako, Mbona mataifa wamefanya ghasia, Na makabila wametafakari ubatili?***

***[26] Wafalme wa dunia wamejipanga, Na wakuu wamefanya shauri pamoja***

***Juu ya Bwana na juu ya Kristo wake.***

***[27] Maana ni kweli, Herode na Pontio Pilato pamoja na Mataifa na watu wa Israeli, walikusanyika katika mji huu juu ya Mtumishi wako mtakatifu Yesu, uliyemtia mafuta,***

***[28] ili wafanye yote ambayo mkono wako na mashauri yako yamekusudia tangu zamani yatokee.***

Hapo amenukuu Zaburi

***Zaburi 2:1-2***

***[1] Mbona mataifa wanafanya ghasia, Na makabila wanatafakari ubatili?***

***[2] Wafalme wa dunia wanajipanga, Na wakuu wanafanya shauri pamoja, Juu ya BWANA, Na juu ya masihi wake,***

Na wanatafsiri ya kuwa hayo siyo Maneno tu ambayo Daudi alijisikia kusemasema... HAPANA... Ni mateso ya Kristo.

Yaani masihi aliyetajwa na Daudi ni KRISTO na wafalme wa dunia ni Herode, na Pontio Pilato...

***Matendo ya Mitume 4:27-28***

***[27] Maana ni KWELI, HERODE NA PONTIO PILATO PAMOJA NA MATAIFA NA WATU WA ISRAELI, walikusanyika katika mji huu juu ya Mtumishi wako mtakatifu Yesu, ULIYEMTIA MAFUTA,***

***[28] ili wafanye yote ambayo mkono wako na mashauri yako yamekusudia tangu zamani yatokee.***

UKIENDA mlango wa 7 Utaona namna Stefano alivyohubiri…

***Matendo ya Mitume 7:2***

***[2] Naye akasema, Ndugu zangu na baba zangu, sikilizeni: Mungu wa utukufu alimtokea baba yetu Ibrahimu, alipokuwa katika Mesopotamia, kabla hajakaa Harani***,

Alianza Kitabu cha Mwanzo… _

***Mwanzo 12:1***

***[1] BWANA akamwambia Abramu, Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha;***

Akaendelea hatua kwa hatua akafika kitabu cha Kutoka angalia alivyonukuu... ***Matendo ya Mitume 7:15***

***[15] Basi Yakobo akashuka mpaka Misri; akafa yeye na baba zetu;***

Akaendelea kuelezea misheni ya Musa Misri na jinsi walivyotoka kisha unabii wa Musa kwa habari ya Kristo...

***Matendo ya Mitume 7:37***

***[37] Musa huyo ndiye aliyewaambia Waisraeli, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye.***

(Hii tumeona sura ya 3).

Musa ALIENDELEA kuchambua maandiko matakatifu na mwishowe alipigwa mawe... lakini alihubiri kwa kuchambua maandiko ya Agano la Kale.

Petro alipokuwa kwa Kornelio alihubiri na kusisitiza kuwa MANABII WOTE walihubiri habari za Kristo.

***Matendo ya Mitume 10:39-43***

***[39] Nasi tu mashahidi wa mambo yote aliyoyatenda katika nchi ya Wayahudi na katika Yerusalemu; ambaye walimwua wakamtundika mtini.***

***[40] Huyo Mungu alimfufua siku ya tatu, akamjalia kudhihirika,***

***[41] si kwa watu wote, bali kwa mashahidi waliokuwa wamekwisha kuchaguliwa na Mungu, ndio sisi, tuliokula na kunywa pamoja naye baada ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu.***

***[42] Akatuagiza tuwahubiri watu na kushuhudia ya kuwa huyu ndiye aliyeamriwa na Mungu awe Mhukumu wa walio hai na wafu.***

***[43] HUYO MANABII WOTE HUMSHUHUDIA, ya kwamba kwa JINA LAKE KILA AMWAMINIYE ATAPATA ONDOLEO LA DHAMBI.***

Paulo alipokuwa kwenye sinagogi akapewa nafasi ya kuhubiri alianza pia kuchambua Agano la Kale...

***Matendo ya Mitume 13:16-23***

***[16] Paulo akasimama, akawapungia mkono, akasema, Enyi waume wa Israeli, nanyi mnaomcha Mungu, sikilizeni.***

***[17] Mungu wa watu hawa Israeli aliwachagua baba zetu, akawatukuza watu hao, walipokuwa wakikaa kama wageni katika nchi ya Misri, na kwa mkono ulioinuliwa akawatoa, akawaongoza.***

***[18] Na kwa muda wa miaka kama arobaini akawavumilia katika jangwa.***

***[19] Na alipokwisha kuwaharibu mataifa saba katika nchi ya Kanaani akawapa nchi yao iwe urithi kwa muda wa miaka kama mia nne na hamsini;***

***[20] baada ya hayo akawapa waamuzi hata zamani za nabii Samweli.***

***[21] Hatimaye wakaomba kupewa mfalme; Mungu akawapa Sauli mwana wa Kishi, mtu wa kabila ya Benyamini, kwa muda wa miaka arobaini.***

***[22] Na alipokwisha kumwondoa huyo, akamwinua Daudi awe mfalme wao ambaye alimshuhudia, akisema, Nimemwona Daudi, mwana wa Yese, mtu anayeupendeza moyo wangu, atakayefanya mapenzi yangu yote.***

***[23] Katika uzao wake mtu huyo Mungu amewaletea Israeli Mwokozi, yaani, Yesu, kama alivyoahidi;***

Alipofika kwa Daudi akasema ahadi ya kumpa mtu akae kwenye ufalme wake milele... akili yako inaweza

kuwaza Sulemani... lakini ukweli ni kwamba AHADI ALIYOPEWA DAUDI NI UFUFUO WA YESU KRISTO.

ALIENDELEA kufundisha

***Matendo ya Mitume 13:32-39***

***[32] Na sisi tunawahubiri habari njema ya ahadi ile waliyopewa mababa,***

***[33] ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu ahadi hiyo, kwa kumfufua Yesu; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili,***

***Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa.***

***[34] Tena ya kuwa alimfufua katika wafu, asipate kurudia uharibifu, amenena hivi,***

***Nitawapa ninyi mambo matakatifu ya Daudi yaliyo amini.***

***[35] Kwa hiyo anena na pengine,***

***Hutamwachia Mtakatifu wako kuona uharibifu.***

***[36] Kwa maana Daudi, akiisha kulitumikia shauri la Mungu katika kizazi chake, alilala, akawekwa pamoja na baba zake, akaona uharibifu.***

***[37] Bali huyu aliyefufuliwa na Mungu hakuona uharibifu.***

***[38] Basi, na ijulikane kwenu, ndugu zangu, ya kuwa kwa huyo mnahubiriwa msamaha wa dhambi;***

***[39] na kwa yeye kila amwaminiye huhesabiwa haki katika mambo yale yote asiyoweza kuhesabiwa haki kwa torati ya Musa.***

Kwa hiyo ahadi waliyopewa akina Ibrahimu, Isaka na Yakobo (mababa) siyo watoto kama Isaka, siyo nchi kama Kanaani, ufalme au ahadi nyingi unazoziona (AHADI HIZO AMBAZO ZINAONEKANA NI NYINGI ZILIKUWA ZINAZUNGUMZIA HABARI ZA KRISTO).

Kwa hiyo Daudi aliponukuu

***Zaburi 2:7***

***[7] Nitaihubiri amri; BWANA aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa.***

Huko kusema mimi Leo nimekuzaa ni kutabiri UFUFUO wa Yesu Kristo kutoka kwenye TUMBO LA NCHI NA SIYO TUMBO LA MWANAMKE.

Ndiyo hiyo hiyo Daudi anasema Hutamwacha Mtakatifu wako auone uharibifu.

Ndiyo hayo hayo Isaya anayaita MAMBO MATAKATIFU YA DAUDI.

UFUFUO WA YESU KRISTO.

Kisha akamaliza kuwa kusema Kila amwaminiye Yesu aliyefufuka HUHESABIWA HAKI BURE, SI KWA MATENDO YA SHERIA.

Paulo aliofika Thesalonike pia...

***Matendo ya Mitume 17:2-4***

***[2] Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake, akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa maneno ya maandiko sabato tatu,***

***[3] akiyafunua na kuwaeleza ya kwamba ilimpasa Kristo kuteswa, na kufufuka katika wafu; na ya kwamba, Yesu huyu ninayewapasha ninyi habari zake ndiye Kristo.***

***[4] Wengine miongoni mwao wakaamini, wakashikamana na Paulo na Sila; na Wayunani waliomcha Mungu, wengi sana, na wanawake wenye cheo si wachache.***

Paulo alitumia SABATO TATU... akahojiana nao kwa maneno ya MAANDIKO sabato tatu, AKIYAFUNUA na KUWAELEZA ya kwamba ilimpasa KRISTO KUTESWA, NA KUFUFUKA KATIKA WAFU; na ya

kwamba, Yesu huyu ninayewapasha ninyi habari zake ndiye Kristo.

Paulo wakati anajitetea mbele ya Agripa anasema

***Matendo ya Mitume 26:22-23***

***[22] Basi kwa kuwa nimeupata msaada utokao kwa Mungu nimesimama hata leo hivi nikiwashuhudia wadogo kwa wakubwa, wala sisemi neno ila yale ambayo manabii na Musa waliyasema, kwamba yatakuwa;***

***[23] ya kwamba Kristo hana budi kuteswa na ya kwamba yeye kwanza kwa kufufuliwa katika wafu atatangaza habari za nuru kwa watu wake na kwa watu wa Mataifa.***

Angalia haya MANENO... wala SISEMI NENO ila yale ambayo MANABII na MUSA waliyasema, kwamba yatakuwa; ya kwamba KRISTO HANA budi KUTESWA na YA KWAMBA YEYE KWANZA KWA KUFUFULIWA KATIKA WAFU ATATANGAZA HABARI ZA NURU KWA WATU WAKE NA KWA WATU KWA MATAIFA.

Huu ni mjumuisho wa ujumbe mzima wa Agano la Kale... YAANI, Kristo kupata mateso na kufufuka.

Kitabu cha Matendo ya mitume kinaisha kwa Paulo kukaa mahali akifundisha akitumia vitabu vya MUSA NA MANABII akifundisha habari za ufalme (UFUFUO WA YESU KRISTO).

***Matendo ya Mitume 28:23***

***[23] Wakiisha kuagana naye siku, wakamjia katika nyumba aliyokaa, watu wengi sana, akawaeleza kwa taratibu na kuushuhudia ufalme wa Mungu, akiwaonya mambo yake Yesu, kwa maneno ya sheria ya Musa na ya manabii, tangu asubuhi hata jioni.***

Hayo ndiyo mambo yaliyohubiriwa kwenye Matendo ya Mitume, ni mambo yaliyoandikwa kwenye vitabu vya Musa na Manabii (Mwanzo mpaka Malaki).

Huko ndipo walipopatia habari kwamba Kristo atateswa, atafufuka na kwa sababu hiyo Msamaha wa dhambi au WOKOVU au uzima wa milele unapatikana bure kabisa.

SHIDA NI KWAMBA: LEO UKIANGALIA MAMBO WALIYOFUNDISHA MITUME WA YESU KRISTO NA MAMBO TUNAYOFUNDISHA MAKANISANI (SIYO YOTE) LEO UTASIKITIKA SANA. NI VITU VIWILI TOFAUTI.

Tubaki kwenye Fundisho la Mitume - KRISTO.

# SURA YA 17

## *NYARAKA NA AGANO LA KALE*

Kuna Baada ya kuangalia Matendo ya Mitume na namna ilivyotumika kuelezea mambo yaliyotabiriwa katika vitabu vya Agano la Kale (Mwanzo mpaka Malaki) pamoja na kutimizwa kwa

ahadi ya ukombozi wa wanadamu kwa njia ya Yesu Kristo ikiwekwa wazi katika vitabu Vinne vya Injili sasa tuangalie kidogo juu ya mambo yaliyoandikwa kwa ujumla kwenye Nyaraka za Mitume.

Kitabu cha kwanza kabisa Warumi (kulingana na mtiririko) kinaanza hivi....

***Warumi 1:1-2***

***[1] Paulo, mtumwa wa Kristo Yesu, aliyeitwa kuwa mtume, na kutengwa aihubiri INJILI YA MUNGU;***

***[2] ambayo Mungu amekwisha KUIAHIDI kwa kinywa cha manabii wake katika MAANDIKO MATAKATIFU;***

Injili ya Mungu ni ahadi katika Maandiko Matakatifu (Mwanzo mpaka Malaki).

Hii tu inaonyesha kuwa vitabu vya Agano Jipya havipingani na Agano la Kale.

Vitabu vya Agano la Kale ni unabii au ahadi na kwenye Agano Jipya wanawasilisha utimilifu wa Ahadi hiyo kwa kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo.

Ndiyo maana Paulo anaendelea kwa kusema...

***Warumi 1:3-4***

***[3] yaani, habari za Mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili,***

***[4] na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu;***

Kwa hiyo Injili hiyo ni habari za Mwana wa Mungu (Yesu Kristo).

*Fast Forward*, Paulo ameanza kunukuu vitabu vya Agano la Kale.

Angalia ***Warumi 1:17***

***[17] Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, Mwenye haki ataishi kwa imani.***

KAMA ILIVYOANDIKWA!... WAPI?

***Habakuki 2:2-4***

***[2] BWANA akanijibu, akasema, Iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji.***

***[3] Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia.***

***[4] Tazama, roho yake hujivuna, haina unyofu ndani yake; lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake.***

Kwa hiyo njozi ya Habakuki ni IMANI KATIKA KRISTO.

Hii imerudiwa pia kwenye

***Waebrania 10:37-38***

***[37] Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, YEYE AJAYE ATAKUJA, wala hatakawia.***

***[38] Lakini MWENYE HAKI WANGU ATAISHI KWA imani; Naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye.***

Mwandishi wa Waebrania ananukuu unabii au njozi ya Habakuki lakini anaonyesha AJAYE NI MTU. HATAKAWIA... BILA SHAKA NI KRISTO.

Angalia Paulo kwa ***Wagalatia 3:11-12***

***[11] Ni dhahiri ya kwamba hakuna mtu ahesabiwaye haki mbele za Mungu katika sheria; kwa sababu Mwenye haki ataishi kwa imani.***

***[12] Na torati haikuja kwa imani, bali, Ayatendaye hayo ataishi katika hayo.***

Kwenye 11 anamnukuu Habakuki na kisha ananukuu kwenye mstari wa 12 kutoka kwenye ***Mambo ya Walawi 18:5***

***[5] Kwa ajili ya hayo mtazishika amri zangu na hukumu zangu; ambazo mtu akizitumia ataishi kwa hizo; mimi ndimi BWANA.***

Paulo anarudia kwenye ***Warumi 10:5***

***[5] Kwa maana Musa aliandika juu ya haki itokayo kwa sheria, ya kuwa, Mtu afanyaye hiyo ataishi kwa hiyo.***

Hii inaonyesha kuwa FUNDISHO LA HAKI KWA IMANI NI FUNDISHO LA MUSA PIA, NA MUSA PIA ALIANDIKA JUU HAKI IPATIKANAYO KWA SHERIA.

Kwenye Warumi 4 Paulo anaendelea kufundisha kutokea kitabu cha Mwanzo...

Haki kwa imani kwa Ibrahimu...

***Warumi 4:1-3***

***[1] Basi, tusemeje juu ya Ibrahimu, baba yetu kwa jinsi ya mwili?***

***[2] Kwa maana ikiwa Ibrahimu alihesabiwa haki kwa ajili ya matendo yake, analo la kujisifia; lakini si mbele za Mungu.***

***[3] Maana maandiko yasemaje? Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki***.

Wala Paulo hakuyachukua hayo maneno hewani bali kwenye

***Mwanzo 15:5-6***

***[5] Akamleta nje, akasema, Tazama sasa mbinguni, kazihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu. Akamwambia, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.***

***[6] Akamwamini BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki.***

Angalia kutoka kwenye ***Warumi 5:12-14***

***[12] Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi;***

***[13] maana kabla ya sheria dhambi ilikuwamo ulimwenguni, lakini dhambi haihesabiwi isipokuwapo sheria;***

***[14] walakini mauti ilitawala tangu Adamu mpaka Musa, nayo iliwatawala hata wao wasiofanya dhambi ifananayo na kosa la Adamu, aliye mfano wake yeye atakayekuja.***

Paulo anaendelea kuchambua maandiko matakatifu hapa anaonyesha chanzo cha dhambi na MAUTI kwenye kitabu cha Mwanzo.

Kisha cha Eliya na manabii wa Baali pia kimerekodia kwenye Warumi

***Warumi 11:3-4***

***[3] Bwana, wamewaua manabii wako, wamezibomoa madhabahu zako, nami nimesalia peke yangu, nao wananitafuta roho yangu.***

***[4] Lakini ile jawabu ya Mungu yamwambiaje? Nimejisazia watu elfu saba wasiopiga goti mbele ya Baali.***

Tena ametoa kwenye ***1 Wafalme 19:14,18***

***[14] Akasema, Nimeona wivu mwingi kwa ajili ya BWANA, Mungu wa majeshi; kwa kuwa wana wa Israeli wameyaacha maagano yako, na kuzivunja madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga; nami nimesalia, mimi peke yangu; nao wanitafuta roho yangu waiondoe.***

***[18] Pamoja na hayo nitajisazia katika Israeli watu elfu saba, kila goti lisilomwinamia Baali, na kila kinywa kisichombusu.***

Kwa hiyo nimeweka Mistari kadhaa kama USHAHIDI kukuonyesha kuwa Vitabu vya Mitume (Nyaraka ni uchambuzi wa vitabu vya Agano la Kale) kwa jicho la Kristo.

Akina Paulo hawakuokota mafundisho yao kwenye hisia zao au kwa kusema nina mafunuo mapya. Yote WALIYOYASEMA na kuandika yanakubaliana na maandiko matakatifu.

Huku ndiko KUHESHIMU maandiko matakatifu.

Hauna mamlaka makubwa ya kutafsiri maandiko matakatifu kwa jinsi unavyopenda isipokuwa kwa jinsi mitume walivyofanya.

## WARAKA WA KWANZA KWA WAKORINTHO

Katika sehemu hii tunaweza tukaangalia kwa sehemu Waraka wa kwanza wa Paulo kwa Wakorintho.

*Fast forward* sura ya kwanza, Paulo anaanza kufundisha akitokea tena kwenye vitabu vya Agano la Kale...

***1 Wakorintho 1:18-21***

***[18] Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu.***

***[19] Kwa kuwa imeandikwa,***

***Nitaiharibu hekima yao wenye hekima,***

***Na akili zao wenye akili nitazikataa.***

***[20] Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mlete hoja wa zamani hizi? Je! Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu?***

***[21] Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa.***

KWA KUWA IMEANDIKWA... WAPI?

Angalia alipotolea...

***Isaya 29:13-14***

***[13] Bwana akanena, Kwa kuwa watu hawa hunikaribia na kuniheshimu kwa vinywa vyao, bali mioyo yao wamefarakana nami, na kicho chao walicho nacho kwangu ni maagizo ya wanadamu waliyofundishwa;***

***[14] kwa sababu hiyo mimi nitafanya tena kazi ya ajabu kati ya watu hawa, kazi ya ajabu na mwujiza; na akili za watu wao wenye akili zitapotea, na ufahamu wa wenye busara wao utafichwa.***

Hii ni kusema watu wanajitahidi kumwabudu Mungu huku wakiikataa Injili ya Yesu Kristo wanatembea katika hekima ya kibinadamu na kukataa hekima ya Mungu iokoayo.

Siyo kwa Isaya tu lakini pia

***Yeremia 8:8-9***

***[8] Mwasemaje, Sisi tuna akili, na torati ya BWANA tunayo pamoja nasi? Lakini, tazama, kalamu yenye uongo ya waandishi imeifanya kuwa uongo.***

***[9] Wenye hekima wametahayari, wamefadhaika na kushikwa; tazama, wamelikataa neno la BWANA, wana akili gani ndani yao?***

WAMELIKATAA NENO LA BWANA

Paulo anaendelea kusema kuwa IMEANDIKWA...

***1 Wakorintho 1:31***

***[31] kusudi, kama ilivyoandikwa, Yeye aonaye fahari na aone fahari juu ya Bwana.***

IMEANDIKWA WAPI?

***Yeremia 9:23-24***

***[23] BWANA asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake;***

***[24] bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua, ya kuwa mimi ni BWANA, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema BWANA,***

Anaendelea kuandika… _

***1 Wakorintho 2:9***

***[9] lakini, kama ilivyoandikwa, Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.***

UKIANGALIA huu mstari unafanana kwa ukaribu sana kwenye Isaya

***Isaya 64:4***

***[4] Maana tangu zamani za kale watu hawakusikia, wala kufahamu kwa masikio, wala jicho halikuona Mungu, ila wewe, atendaye mambo kwa ajili yake amngojaye.***

Kwenye 1 Wakorintho 5:7

***[7] Basi, jisafisheni, mkatoe ile chachu ya kale, mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani, Kristo;***

Paulo anajikita kuzungumzia mwenendo wa Waamini kwa kutumia maandiko ya Agano la Kale.

CHACHU YA KALE

PASAKA

Hizi ni lugha za Musa... zikiwa na maana ya kivuli cha Kristo.

***Kutoka 12:15***

***[15] Mtakula mikate isiyochachwa muda wa siku saba; siku hiyo ya kwanza mtaondoa chachu yote isiwe katika nyumba zenu kabisa; kwa kuwa mtu ye yote atakayekula mkate uliochachwa tangu siku hiyo ya kwanza hata siku ya saba, nafsi hiyo atakatiliwa mbali na Israeli.***

***Kumbukumbu la Torati 16:3***

***[3] Usimle pamoja na mikate iliyotiwa chachu; siku saba utakula naye mikate isiyotiwa chachu, nayo ni mikate ya mateso; kwa maana ulitoka nchi ya Misri***

***kwa haraka; ili upate kukumbuka siku uliyotoka nchi ya Misri, siku zote za maisha yako.***

ANATUMIA MIFANO YA AGANO LA KALE KUFUNDISHA JUU YA KUSHUGHULIKA NA SWALA LA UZINZI.

Anaendelea ***1 Wakorintho 6:14***

***[14] Naye Mungu alimfufua Bwana, na tena atatufufua sisi kwa uweza wake.***

Hili tunaliona kwa mapana katika vitabu vinne vya Injili.

Paulo anaendelea...

***1 Wakorintho 6:16-17***

***[16] Au hamjui ya kuwa yeye aliyeungwa na kahaba ni mwili mmoja naye? Maana asema, Wale wawili watakuwa mwili mmoja.***

***[17] Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye.***

Hapa anatumia mfano wa ndoa ya **Mwanzo 2:24** kufundisha kwamba Waamini wameungwa pamoja na Bwana na hivyo hawatakiwi kuwa na ndoa na WASIOAMINI.

Hii imetoka ***Mwanzo 2:24***

***[24] Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.***

Kuwa Mwili Mmoja (Musa) = Kuwa roho moja (Paulo)

Habari hii pia Paulo aliandikwa kwa Waefeso

***Waefeso 5:30-31***

***[30] Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake.***

***[31] Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja.***

Paulo anafundisha UTOAJI kwa kutumia vitabu vya Musa...

Angalia, ***1 Wakorintho 9:7***

***[7] Ni askari gani aendaye vitani wakati wo wote kwa gharama zake mwenyewe? Ni nani apandaye mizabibu asiyekula katika matunda yake? Au ni nani achungaye kundi, asiyekunywa katika maziwa ya kundi?***

ASKARI

ZABIBU NA

KUNDI...

KAYATOA WAPI?

ANGALIA, ***Kumbukumbu la Torati 20:6***

***[6] Ni mtu gani aliye hapa aliyepanda shamba la mizabibu, wala hajatumia matunda yake? Aende akarudi nyumbani kwake asije akafa mapiganoni, yakatumiwa na mtu mwingine matunda yake.***

TENA ***Mithali 27:18***

***[18] Yeye autunzaye mtini atakula matunda yake; Naye amhudumiaye bwana wake ataheshimiwa.***

Paulo anaendelea kukazia

***1 Wakorintho 9:8-11***

***[8] Je! Ninanena hayo kwa kibinadamu? Au torati nayo haisemi yayo hayo?***

***[9] Kwa maana katika torati ya Musa imeandikwa,_ _U_S_I_M_F_U_N_G_E_ _K_I_N_Y_W_A_ _n_g_'o_m_b_e_ _A_P_U_R_A_P_O_ _N_A_F_A_K_A_._ _J_e_!_ _H_a_p_o_ _M_u_n_g_u_ _a_a_n_g_a_l_i_a_ _m_a_m_b_o_ _y_a_ _n_g_'o_m_b_e_?_ _***

***[10] Au yamkini anena hayo kwa ajili yetu? Naam, yaliandikwa kwa ajili yetu; kwa kuwa alimaye nafaka ni haki yake kulima kwa matumaini, naye apuraye nafaka ni haki yake kutumaini kupata sehemu yake.***

***[11] Ikiwa sisi tuliwapandia ninyi vitu vya rohoni, je! Ni neno kubwa tukivuna vitu vyenu vya mwilini?***

Paulo anaelewa kuwa Musa alikuwa haanndiki juu ya ng'ombe bali watu.

Iko hapa**....** ***Kumbukumbu la Torati 25:4***

***[4] N_g_'o_m_b_e_ _a_p_u_rapo nafaka usimfunge kinywa.***

Paulo pia ametumia kwa Timotheo

ANGALIA ***1 Timotheo 5:17-18***

***[17] Wazee watawalao vema na wahesabiwe kustahili heshima maradufu; hasa wao wajitaabishao kwa kuhutubu na kufundisha.***

***[18] Kwa maana andiko lasema, Usimfunge kinyw_a_ _n_g_'o_m_b_e_ _a_p_u_r_a_p_o_ _n_a_f_a_k_a_._ _N_a_ _tena, Mtenda kazi astahili ujira wake.***

Paulo anaendelea kuchambua Agano la Kale akifundisha juu ya kuwasaidia wahudumu wa injili...

***1 Wakorintho 9:13-14***

***[13] Hamjui ya kuwa wale wazifanyao kazi za hekaluni hula katika vitu vya hekalu, na wale waihudumiao madhabahu huwa na fungu lao katika vitu vya madhabahu?***

***[14] Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili.***

Haya ameyatoa wapi?

***Mambo ya Walawi 6:16,26***

***[16] Na unga uliosalia Haruni na wanawe wataula; utaliwa pasipo kutiwa chachu, katika mahali patakatifu; katika ua wa hema ya kukutania ndipo watakapoula.***

***[26] Huyo kuhani atakayeisongeza kwa ajili ya dhambi ndiye atakayeila; italiwa katika mahali patakatifu, katika ua wa hema ya kukutania.***

Tena

***Mambo ya Walawi 7:6***

***[6] Kila mtu mume miongoni mwa makuhani atakula katika sadaka hiyo; italiwa katika mahali patakatifu; ni takatifu sana.***

***Hesabu 5:9-10***

***[9] Tena kila sadaka ya kuinuliwa, ya vitu vitakatifu vya wana wa Israeli, watakavyosongeza kwa kuhani, itakuwa ni yake.***

***[10] Tena vitu vilivyowekwa wakfu na mtu awaye yote, vitakuwa ni vya kuhani; kitu cho chote mtu atakachompa kuhani, kitakuwa chake.***

Hizi ni baadhi ya sehemu Paulo anaweza kuchukua hili la kuwategemeza WAHUDUMU wa Injili (Wazee watawalao vema).

SASA UKIENDELEA KATIKA SURA ZILIZOBAKI UTAONA JINSI PAULO ALIPOKUWA AKITOA MAELEKEZO KATIKA KANISA LA KORINTHO KWA KUTUMIA MAANDIKO YA AGANO LA KALE.

**MAMBO MUHIMU NI KWAMBA:**

**1. MAMBO YALIYOKO KWENYE NYARAKA YAKO KWENYE AGANO LA KALE.**

**2. MAMBO HAYO HAWAKUCHUKUA KAMA ILIVYOANDIKWA BALI WALIYATAFSIRI.**

**3. HII HUTUONYESHA KUWA AGANO LA KALE NI LUGHA ZA VIFICHO LAKINI NYARAKA NI TAFSIRI YA WAZI. (mfano: Usimfunge ng'ombe kinywa apurapo nafaka NI SAWA NA KUSEMA Usiache kukutana na mahitaji ya kimwili ya MHUDUMU ANAYEKUHUDUMIA) ANGALI HIYO TAFSIRI.**

**4. BIBLIA NI INA UJUMBE MMOJA ILA LUGHA INAWEZA KUWA TOFAUTI KWENYE SEHEMU TOFAUTI.**

**5. MITUME HAWAKUFUNDISHA MWENENDO WA WATAKATIFU KUTOKA HEWANI BALI WALICHAMBUA AGANO LA KALE. (Ndoa, usafi, Maneno, maombi, utoaji, karama za Roho, n.k.)**

# WARAKA WA PILI KWA WAKORINTHO

Sasa tuangalie waraka wa pili kwa Wakorinto.

***2 Wakorintho 2:15-16***

***[15] Kwa maana sisi tu manukato ya Kristo, mbele za Mungu, katika wao wanaookolewa, na katika wao wanaopotea;***

***[16] katika hao wa pili harufu ya mauti iletayo mauti; katika hao wa kwanza harufu ya uzima iletayo uzima.***

Hapa tunaona jinsi mwandishi alivyowaelezea Waamini kuwa wamefanyika manukato (harufu nzuri sana) mbele za Mungu kupitia Kristo Yesu. Hii tafsiri ilikuwa ni ufafanuzi wa unabii wa Ezekieli akisema; -

***Ezekieli 20:41***

***[41] Nitawatakabali kama harufu ipendezayo, nitakapowatoa katika mataifa, na kuwakusanya toka nchi zile mlizotawanyika; nami nitatakaswa kwenu machoni pa mataifa.***

***[42] Nanyi mtajua ya kuwa mimi ndimi BWANA, nitakapowaingiza katika nchi ya Israeli, katika nchi ile ambayo niliuinua mkono wangu kwamba nitawapa baba zenu.***

Wote tunafahamu kuwa nchi ambayo Mungu aliinua mkono wake akiahidi kuwapa mababa wa kale ilikuwa ni Kristo kufanyika makao ya waamini yaani UKOMBOZI

***2 Wakorintho 3:2-3***

***[2] Ninyi ndinyi barua yetu, iliyoandikwa mioyoni mwetu, inajulikana na kusomwa na watu wote;***

***[3] mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tuliyoikatibu, iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa Mungu aliye hai; si katika vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama.***

Tunaona Paulo akitumia lugha ya Musa (lugha ya picha) katika kuelezea hali ya mioyo ya watu yaan wale waliokubali mioyo yao kusomeka kupitia Kristo.

Akimaanisha; -

-Vibao, moyo wa nyama, WALIOAMINI.

-Vibao vya mawe, WASIOAMINI

Anaendelea tena mistari ya mbele kidogo;-

***2 Wakorintho 3:6-9***

***[6] Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya; si wa andiko, bali wa roho; kwa maana andiko huua, bali roho huhuisha.***

***[7] Basi, ikiwa huduma ya mauti, iliyoandikwa na kuchorwa katika mawe, ilikuja katika utukufu, hata Waisraeli hawakuweza kuukazia macho uso wa Musa, kwa sababu ya utukufu wa uso wake; nao ni utukufu uliokuwa ukibatilika;***

***[8] je! Huduma ya roho haitazidi kuwa katika utukufu?***

***[9] Kwa maana ikiwa huduma ya adhabu ina utukufu, siuze huduma ya haki ina utukufu unaozidi.***

Hapa tunaona maneno yafuatayo yakitumika: -

- Andiko/huduma ya mauti/huduma ya adhabu

- Roho/huduma ya roho/huduma ya Haki.

Haya mambo yote Paulo ameyatoa wapi? Ngoja tuone

Kwenye version ya Amplified Bible inasomeka hivi: -

***2Corinthians.3.6***

***- [It is He] Who has qualified us [making us to be fit and worthy and sufficient] as ministers and dispensers of a new covenant [of salvation through Christ], not [ministers] of the letter (of legally written code) but of the Spirit; for the code [of the Law] kills, but the [Holy] Spirit makes alive.***

Ile maana ya andiko hapo imetafsiriwa **kama** ***letter~a legally written code*** ambayo kwa kiswahili tungesema ***hati ya kisheria*** iliyoandikwa.

Paulo lazima alikuwa amesoma hapa: -

***Kutoka 32:15***

***[15] Basi, Musa akageuka akashuka katika mlima, na zile mbao mbili za mawe mikononi mwake; mbao zilizoandikwa pande zote mbili, upande huu na upande huu ziliandikwa.***

...Akionesha kuwa kilichokuwa kimeandikwa hapo, torati~andiko, hakikuwa na uzima ndani yake (mwanadamu kuweza kujipatanisha na Mungu) ila mauti (mwanadamu kutenganishwa na Mungu).

Hivyo kusema Huduma ya Mauti/ Huduma ya adhabu ni kuonyesha uhalisia wa Torati katika kuwakamilisha watu na Huduma ya roho/ Huduma ya haki ni kuonyesha uhalisia ya kazi kamilifu ya ukombozi katika kuwakamilisha watu.

Anaendelea tena: -

***2 Wakorintho 12-16***

***[12] Basi, kwa kuwa mna taraja la namna hii, twatumia ujasiri mwingi;***

***[13] nasi si kama Musa alivyotia utaji juu ya uso wake, ili kwamba Waisraeli wasitazame sana mwisho wa ile iliyokuwa ikibatilika;***

***[14] ila fikira zao zilitiwa uzito. Kwa maana hata leo hivi, wakati lisomwapo Agano la Kale, utaji uo huo wakaa; yaani, haikufunuliwa kwamba huondolewa katika Kristo;***

***[15] ila hata leo, torati ya Musa isomwapo, utaji huikalia mioyo yao.***

***[16] Lakini wakati wo wote watakapomgeukia Bwana, ule utaji huondolewa.***

Bila shaka mwandishi alitafsiri kutokea hapa; -

***Kutoka 34:29-30,33***

***[29] Hata ikawa, Musa aliposhuka katika mlima Sinai, na zile mbao mbili za ushuhuda zilikuwa mkononi mwa Musa, hapo aliposhuka katika mlima, Musa hakujua ya kuwa_ _n_g_o_z_i_ _y_a_ _u_s_o_ _w_a_k_e_***

***_i_l_i_n_g_'a_a_ _k_w_a_ _s_a_b_a_b_u_ _a_m_e_s_e_m_a_ _n_a_y_e_._ _***

***[30] Basi Haruni na wana wote wa Israeli walipomwona Musa, tazama, ngozi ya uso w_a_k_e_ _i_l_i_n_g_'a_a_;_ _n_a_o_ _w_a_k_a_o_g_o_p_a_ _k_u_m_k_a_r_i_b_i_a_._ _***

***[33] Na Musa alipokuwa amekwisha kusema nao, akatia utaji juu ya uso wake.***

Sasa Paulo ametoa ufafanuzi zaidi kuwa shida yao haikuwa utaji (coverage) uliokuwa unafunika uso wa Musa ila shida ilikuwa kwenye fikra (moyo) kutiwa uzito kwa kutokuelewa mafundisho ya Musa ndio maana Musa akaweka utaji juu yake.

Ndio maana jinsi Musa alivyokuwa anamuelewa Mungu ni tofauti kabisa na waisraeli.

Mwandishi wa Zaburi anathibitisha hili kwa kuandika hivi: -

***Zaburi 103:7***

***[7] Alimjulisha Musa njia zake, Wana wa Israeli matendo yake.***

Njia za Mungu (asili yake halisi) zilikuwa wazi kwa Musa lakini waisraeli walikataa kuzielewa wakaishia

kuyaelewa matendo yake tu (His response towards unbelief)

Kumbe sio kwamba Mungu alikuwa anajificha ili wasimjue (utaji kufunika uso wa Musa) ila ugumu wa mioyo yao kutotaka kujua ndio ukapeleke Musa kujiwekea utaji.

Mwandishi (Paulo) ameonesha kuwa bado kuna watu katika Korintho walikuwa wanasoma agano la kale wakikaliwa na utaji kwenye mioyo yao, bila kufahamu kuwa huondolewa katika Kristo.

Yaani kwa KUMUAMINI KRISTO, ufahamu wote wa Mungu unakuwa wazi ndani ya mioyo ya watu.

Tuendelee tena…

***2 Wakorintho 6:1-2***

***[1] Nasi tukitenda kazi pamoja naye twawasihi msiipokee neema ya Mungu bure.***

***[2] (Kwa maana asema, Wakati uliokubalika nalikusikia, Siku ya wokovu nalikusaidia; tazama, wakati uliokubalika ndio sasa; tazama, siku ya wokovu ndiyo sasa.)***

Hapa Paulo alinukuu kile ambacho nabii Isaya alisema kuonyesha utayari wa moiyo kuipokea INJILI pindi inapohubiriwa. (KUAMINI NI SASA)

Isaya aliandika hivi: -

***Isaya 49:8***

***[8] BWANA asema hivi, Wakati uliokubalika nimekujibu, na siku ya wokovu nimekusaidia; nami nitakuhifadhi, nitakutoa uwe agano la watu hawa, ili kuiinua nchi hii, na kuwarithisha urithi uliokuwa ukiwa;***

***2 Wakorintho 6:17-18***

***[17] Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha.***

***[18] Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi.***

Paulo ameyachukua maneno hayo kutoka kwa;

- Musa

***Mambo ya Walawi 26:12***

***[12] Nami nitakwenda kati yenu, nami nitakuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu wangu.***

- Na Nabii Isaya

***Isaya 52:11***

***[11] Nendeni zenu, nendeni zenu, tokeni huko, msiguse kitu kichafu; tokeni kati yake; iweni safi ninyi mnaochukua vyombo vya BWANA.***

Akifafanua utimilifu wa Ahadi ya Mungu, kwa wote watakaoamini INJILI kutengwa na kuwa ushirika mmoja na Mungu.

***2 Wakorintho 9:8-9***

***[8] Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema;***

***[9] kama ilivyoandikwa, Ametapanya, amewapa maskini, Haki yake yakaa milele.***

Hapo Paulo amenukuu kutoka kwenye Zaburi…

***Zaburi 112:9***

***[9] Amekirimu, na kuwapa maskini, Haki yake yakaa milele, Pembe yake itatukuzwa kwa utukufu***.

Akifafanua jinsi ambavyo mwamini ametajirishwa katika upya wa roho yake ili nae pia aweze kuwatajirisha wengine.

Utajiri wa Mwamini ni katika kupokea: -

-Msamaha wa dhambi wa milele.

-Kukaliwa na Roho mtakatifu milele.

-Kuwa na Uzima wa milele.

-Kufanyika makao ya Mungu.

Na kuwapa wengine utajiri huo ni KUWAHUBIRIA INJILI.

***2 Wakorintho 12:7-10***

***[7] Na makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi, kwa wingi wa mafunuo hayo nalipewa mwiba katika mwili, mjumbe wa Shetani ili anipige, nisije nikajivuna kupita kiasi.***

***[8] Kwa ajili ya kitu hicho nalimsihi Bwana mara tatu kwamba kinitoke.***

***[9] Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu.***

***[10] Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu.***

Kutumia maneno nalipewa mwiba... Paulo alikuwa anamaanisha nini?

Hebu soma hapa…

***Ezekieli 28:24***

***[24] Wala hautakuwapo mchongoma uchomao kwa nyumba ya Israeli; wala mwiba uumizao miongoni mwa wote wamzungukao, waliowatenda mambo ya jeuri; nao watajua ya kuwa mimi ndimi Bwana MUNGU.***

Hapo Ezekieli ametumia lugha ya mchongoma na mwiba kuonyesha watu walikuwa kinyume na taifa la israeli.

Lugha hiyo pia Paulo ndio ameitumia kusema Nalipewa mwiba… _yaani watu waliokuwa wanapinga Huduma yake ya injili, ndio sababu mstari wa 10 anamalizia kusema Napendezwa na misiba, adha, shida wa ajili ya Kristo... Yote hayo ni ufafanuzi kuwa kwa ajili ya Kristo yaan INJILI, Paulo amekuwa akipata misukosuko kutoka kwa watu, wapinzani lakini anaweka wazi kuwa katikati ya hayo yote yeye bado ni mwenye nguvu za kuendelea kumhubiri KRISTO.

***2 Wakorintho 13:1***

***[1] Hii ndiyo mara ya tatu ya mimi kuja kwenu. Kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno litathibitishwa.***

Hata Kusema hivyo tu, Paulo alinukuu kutoka kwa Musa;

***Kumbukumbu la Torati 17:6***

***[6] Huyo atakayeuawa na auawe kwa midomo ya mashahidi wawili, au mashahidi watatu; asiuawe kwa mdomo wa shahidi mmoja.***

Ufahamu huu unatupa KUAMINI kuwa maandiko yanajitafsiri yenyewe na yamebeba ujumbe mmoja.

Yalioandikwa hasa katika Nyaraka zote yalinukuliwa kutoka kwenye maandiko ya Agano la kale.

ITAENDELEA…..

## Vitabu Vingine vya Shemeji Melayeki

1. *Principles for Greatness*
2. *Principles of Growth*
3. *The Power of Vision*
4. *The Power of Taking the First Step*
5. *The Power of Reading Books*
6. *Nguzo za Siku: Msingi wa Kwanza*
7. *Nguzo za Siku: Msingi wa Pili*
8. *Ukombozi Reloaded*
9. *Utajiri wa Ukoo*
10. *Siku 14 za Maajabu*
11. *Kufunga Reloaded*
12. *Kabla Ya Kuomba*

Shemeji Melayeki ni muasisi wa huduma ya Global Family Gatherings Ministries na mnenaji katika makongamano mbalimbali. Yeye, mke wake na watoto wanaishi jijini Dar es Salaam.

Kwa maombi au ushauri tumia anuani zifuatazo.

Email: *shemeji.melayeki@gmail.com*
Instagram: *apostle_shemeji_melayeki*
Facebook: *Apostle Shemeji Melayeki*
YouTube: *Ap Shemeji Melayeki*
Twitter: *@melayeki*

Kufika kwenye ibada zetu na kambi za mafundisho ya neno la Mungu tumia simu +255 714 548 565.

Unaweza kujiunga na vikundi vya mafundisho kwa njia ya mitandao kwa namba hiyo hiyo.

Ukitaka kuwa sehemu ya watu wanaowekeza fedha zao katika kutusaidia kufika injili kwa watu wengine kwa njia ya maandishi na redio tumia +255 763 965 297.

# UMEBARIKIWA!